

ITHIBATI

Aliyetia saina hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii yenye anuani “**Maana Fiche ya Maneno Yanayotumiwa na Waathirika wa Dawa za Kulevya Zanzibar**” na ameridhia kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

.....

Dkt. Masoud Nassor Mohammed

Msimamizi

.....

Tarehe

TAMKO

Mimi *Saada Juma Ramadhan* ninathibitisha kwamba, tasnifu hii ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au shahada nyingine yoyote.

.....
Saini

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Tasnifu hii inalindwa na sheria za hakimiliki za kitaifa na kimataifa. Hairuhusiwi kwa namna yoyote ile kunakili kazi yote au sehemu ya kazi hii bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar isipokuwa kutumia sehemu ndogo kwa lengo la utafiti au kujisomea au kufanya uchambuzi yakinifu wa kitaaluma.

SHUKURANI

Kwanza kabisa ninatoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu mtukufu aliyenijaalia uhai, nguvu, fikra na uwezo wa kuandika na kukamilisha kazi hii. Kwa hakika bila msaada wake lolote haliwezi kufanyika. Tasnifu hii imekamilika kutokana na msaada mkubwa wa Allah Subhanahu Wataala.

Shukurani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt. Masoud Nassor Mohammed kwa kubeba jukumu la kusimamia vyema kazi hii. Ninamshukuru kwa ujasiri na uvumilivu wake mkubwa tokea hatua ya kuandika pendekezo la utafiti hadi kumalizika kwa kazi hii. Ninaamini kuwa amevumilia vya kutosha udhaifu wangu kama binaadamu na kama mwanafunzi. Kukamilika kwa tasnifu hii kumetokana na juhudi yake kubwa ya kusoma, kukosoa, kurekebisha, kuelekeza na kushauri yale yote yanayofaa kuzingatiwa katika utafiti huu. Ingawa ana majukumu mengi hakisita kusoma kazi yangu na kutoa maelekezo yanayojenga kwa umakini mkubwa. Sina cha kumlipa namuombea kwa Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu na amzidishie nguvu na imani ili aweze kutoa mchango wake wa kitaaluma zaidi na atakapomaliza uhai wake hapa duniani Mwenyezi Mungu amridhie huko aendako.

Aidha, ninapenda kuushukuru uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar hasa Idara ya Kiswahili na Kurugenzi ya Masomo ya Juu, Utafiti na Ushauri kwa muongozo na usimamizi mzuri wa masomo yangu. Ninawashukuru pia wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili hasa walimu wangu wapendwa; Dkt Masoud Nassor Mohammed, Dkt Ally

Saleh Khalfan, Dkt Omar Salum Mohamed, Dkt. Zainab Ali Iddi, Prof. Alwiya S. Omar, Prof. Abdul aziz Y. Lodhi na wengineo, bila kumsahau Dkt Salma Omar Hamad; Mhadhiri na Mkurugenzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tawi la Zanzibar. Hawa wote wamenijengea misingi imara katika taaluma hii ya uzamili. Mungu awape maisha ya furaha ili waendeleo kutoa mchango wa kitaaluma na wa kijamii katika taifa letu.

Halikadhalika, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu wote wa shahada ya uzamili ya Kiswahili wa mwaka wa masomo 2018/2019, ushirikiano wao wa dhati walionipatia katika masuala ya kitaaluma kwa kipindi chote cha masomo ya uzamili umeniwezesha kukamilisha kazi hii.

Kwa jumla, watu waliotoa mchango wao hadi kumalizika kwa kazi hii ni wengi sana na vigumu kuwataja wote katika wasaa huu. Nawaomba waamini kuwa mchango wao umepokelewa kwa moyo mkunjufu na umesaidia kufanikisha kazi hii. Mwenyezi Mungu awajaze imani na baraka katika maisha yao. Wote kwa ujumla nawaombea kwa Mwenyezi Mungu kheri za dunia na akhera. Amin.

TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa mume wangu; Dk. Ismail Said Gatalya na watoto wetu; Zaydath Ismail Said na Said Ismail Said pamoja na wazazi wangu; Bw. Juma Ramadhan Said na Bi. Hawa Shaaban Kazwika kwa msaada wao wa hali na mali mpaka kukamilika kwa kazi hii.

VIFUPISHO NA ALAMA

+: Mipaka ya silabi au aina za maneno

Bi: Bibi

Bw: Bwana

Dkt: Mtu mwenye elimu ya shahada ya tatu (Uzamivu)

Dk: Daktari wa binaadamu.

LgzK: Lugha za Kigeni

MyK: Maneno ya Kubuni

Na: Namba

NkM: Nadharia Kidhi ya Mawasiliano.

NmM: Nadharia ya Maana ni Matumizi

S.W: Subuahanahu wa Ta’aalaa

TGPSH: Tanzanian German Programme to Support Health

TTKKDKZ: Tume ya Taifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar

TY: Tafsiri yangu

YALIYOMO

ITHIBATI.....	i
TAMKO.....	ii
HAKIMILIKI.....	ii
SHUKURANI.....	iii
TABARUKU.....	v
VIFUPISHO NA ALAMA.....	vi
YALIYOMO.....	vii
ORODHA YA MAJADWELI.....	xi
ORODHA YA MICHORO.....	xiii
IKISIRI.....	xiv
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI.....	1
1.1 Utangulizi wa jumla.....	1
1.2 Usuli wa mada.....	1
1.3 Tatizo la utafiti.....	5
1.4 Malengo ya utafiti.....	5
1.4.1 Lengo kuu.....	5
1.4.2 Malengo mahsusi.....	6
1.5 Maswali ya utafiti.....	6
1.6 Umuhimu wa utafiti.....	6
1.7 Mipaka ya utafiti.....	7
1.8 Hitimisho.....	8
SURA YA PILI.....	9
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA.....	9
2. 1 Utangulizi.....	9
2.2 Kazi tangulizi.....	9
2.2.1 Mapitio ya jumla kuhusu maana za maneno.....	9
2.2.2 Mapitio kuhusu dhana ya dawa za kulevya.....	17

2.3 Kiunzi cha nadharia	21
2.3.1 Nadharia kidhi ya mawasiliano (NkM).....	21
2.3.2 Nadharia ya maana ni matumizi (NmM)	25
2.3 Hitimisho.....	27
SURA YA TATU.....	29
MBINU ZA UTAFITI.....	29
3.1 Utangulizi.....	29
3.2 Mkabala wa utafiti	29
3.3 Eneo la utafiti	29
3.4 Uteuzi wa sampuli.....	30
3.4.1 Sampuli ya utafiti.....	30
3.4.2 Usampulishaji	33
3.5 Mbinu za kukusanyia data	35
3.5.1 Mbinu ya usaili	35
3.5.2 Mjadala wa kundi lengwa	36
3.5.3 Mbinu ya ushuhudiaji	36
3.6 Vifaa vya kukusanyia data	37
3.6.1 Daftari na kalamu.....	37
3.6.2 Kinasa sauti	37
3.6.3 Kompyuta.....	37
3.6.4 Flashi.....	37
3.6.5 Muongozo wa usaili.....	38
3.6.6 Muongozo wa mjadala wa kundi lengwa.....	38
3.7 Mbinu za uchanganuzi wa data.....	38
3.8 Uthabiti na kuaminika kwa data	39
3.8.1 Uthabiti wa mbinu za kukusanyia data	39
3.8.2 Kuaminika kwa data	40
3.9 Miiko na maadili ya utafiti.....	40
3.10 Hitimisho.....	40

SURA YA NNE	41
UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....	41
4.1 Utangulizi.....	41
4.2 Ubainishaji wa maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya	41
4.2.1 Maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya.....	42
4.2.1.1 Miundo ya maneno ya Kiswahili	45
4.2.1.1.1 Muundo wa maneno.....	45
4.2.1.1.1.1 Maneno ambatani ya maneno matatu	45
4.2.1.1.1.2 Maneno ambatani ya maneno mawili	45
4.2.1.1.1.3 Neno moja.....	46
4.2.1.1.2 Aina za maneno ya Kiswahili	47
4.2.1.1.3 Matumizi ya virai.....	48
4.2.1.2 Miundo ya maneno ya kubuni.....	49
4.2.1.2.1 Idadi ya silabi zilizounda maneno ya kubuni.....	49
4.2.1.2.3 Muundo wa silabi katika maneno ya kubuni	52
4.2.1.3 Maneno yenye asili ya lugha za kigeni	53
4.2.1.3.1 Ubainishaji wa matamshi ya maneno	54
4.2.1.3.2 Aina za maneno yenye asili ya lugha za kigeni	55
4.3 Ufafanuzi wa maana fiche za msamiati	56
4.3.1. Aina za dawa za kulevya.....	57
4.3.2. Vipimo vya dawa za kulevya.....	60
4.3.3. Vifungashio vya dawa za kulevya	62
4.3.4. Taasisi zinazopambana na dawa za kulevya.....	64
4.3.5. Wauzaji wa dawa za kulevya.....	66
4.3.6 Kuwadhihaki vijana wasiotumia dawa za kulevya	69
4.4 Sababu za matumizi ya maana fiche.....	71
4.4.1 Sababu za kiusalama	71
4.4.2 Kuweka siri	72
4.4.3 Kuwatia hofu wanajamii	73

4.4.4 Kuogopa unyanyapaa wa wanajamii	74
4.4.5. Kujitofautisha na wanajamii wengine.....	75
4.5. Athari za matumizi ya maana fiche	77
4.5.1. Kuharibu lugha ya kiswahili	77
4.4.2 Mwendelezo wa uingizwaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevywa.....	80
4.5.3 Huathiri harakati za mapambano dhidi ya dawa za kulevywa.....	82
4.5.4 Ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevywa	84
4.5.5 Kuathiri mawasiliano baina ya wahudumu na waathirika wa dawa za kulevywa....	86
4.5.6 Kuharibu utamaduni wa jamii.....	88
4.4.7 Kukuza lugha	89
4.6. Muhtasari wa sura	92
SURA YA TANO	93
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	93
5. 1 Utangulizi.....	93
5.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti.....	93
5.3 Mapendekezo	100
5.3.1 Mapendekezo ya jumla	100
5.3.2 Mapendekezo ya tafiti fuatizi.....	100
5.4 Hitimisho.....	101
MAREJELEO	102
VIAMBATANISHO.....	107

ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Na. 3.1: Ufafanuzi wa Mgawanyo wa Sampuli.....	33
Jadweli Na. 4.1: Asili ya Msamiati	43
Jadweli Na. 4.2: Muundo wa Maneno	46
Jadweli Na. 4.3: Aina za Maneno ya Kiswahili.....	47
Jadweli Na. 4.4: Matumizi yaVirai	48
Jadweli Na. 4.5: Idadi ya Silabi Katika Maneno ya Kubuni.....	50
Jadweli Na. 4.6: Aina za Silabi Katika Maneno ya Kubuni	51
Jadweli Na. 4.7: Muundo wa Silabi Katika Maneno ya Kubuni	52
Jadweli Na. 4.8: Matamshi ya Maneno.....	54
Jadweli Na. 4.9: Aina za Maneno ya Lugha za Kigeni.....	55
Jadweli Na. 4.10: Maana Fiche Katika Majina ya Dawa za Kulevya.....	58
Jadweli Na. 4.11: Majina ya Vipimo vya Dawa za Kulevya	61
Jadweli Na. 4.12: Majina ya Vifungashio vya Bangi	63
Jadweli Na. 4.13: Maneno Yanayohusu Taasisi Zinazopambana na Dawa za Kulevya ..	64
Jadweli Na. 4.14: Majina ya Wauzaji wa Dawa za Kulevya	67
Jadweli Na. 4.15: Majina Yanayotumika Kuwadhihaki Wasiotumia Dawa za Kulevya .	70
Jadweli Na: 4.16: Matokeo ya Sababu za Matumizi ya Maana Fiche	76
Jadweli Na 4.17: Maneno Yenye Maana Fiche Yanayoharibu Lugha	78
Jadweli Na 4.18: Muhtasari wa Watoa Taarifa Walioelezea Namna lugha Inavyoathirika	80

Jadweli Na. 4.19: Muhtasari wa Watoa Taarifa Kuhusu Athari Katika Mapambano ya Dawa za Kulevya	84
Jadweli Na. 4.20: Majina Yanayowadhiki Vijana Wasiotumia Dawa za Kulevya.....	85
Jadweli Na. 4.21: Huharibu Utamaduni wa Jamii	89
Jadweli Na. 4.22: Athari za Maana Fiche za Maneno	91

ORODHA YA MICHORO

Mchoro Na. 2.1 Nadharia kidhi ya mawasiliano	24
Mchoro Na. 2.2 Nadharia ya maana ni matumizi	26
Mchoro Na. 2.3 Nadharia zilivyotumika katika utafiti	27

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza “Maana Fiche ya Maneno Yanayotumiwa na Waathirika wa Dawa za Kulevya Zanzibar”. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Malengo mahsusi ya utafiti huu ni; Kubainisha maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar, kufafanua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar, kujadili sababu za matumizi ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar pamoja na kutathmini athari za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Nadharia ya Maana ni Matumizi iliyoasisiwa na Wittgenstein (1933) na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano ya Giles (1973) zimetumika kuuongoza utafiti huu. Jumla ya watoa taarifa 73 walishirikishwa katika utafiti huu. Data zimekusanywa kwa mbinu ya usaili, mjadala wa kundi lengwa na ushuhudiaji. Uchambuzi wa data umefanywa kwa njia ya maelezo na majadwali yametumika pale ilipohitajika. Jumla ya maneno mia moja na sita (106) yenye maana fiche yamekusanywa na kuchambuliwa. Maana fiche za maneno zimechambuliwa kwa kuzingatia; aina ya dawa za kulevya, Vipimo vya dawa za kulevya na maana fiche zinazohusu taasisi zinazopambana na dawa za kulevya. Vilevile, sababu tano za matumizi ya maana fiche zimebainika; sababu za kiusalama, kutunza siri, kuwatia hofu wanajamii, kuogopa unyanyapaa wa wanajamii na kujitofautisha na wanajamii wengine. Athari sita za matumizi ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar zimejitokeza. Athari hizo ni; kuharibu lugha ya Kiswahili, mwendelezo wa uingizwaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya, kuathiri harakati za mapambano dhidi ya dawa hizo, ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, kuathiri mawasiliano baina ya wahudumu na waathirika wa dawa za kulevya na kuipotosha jamii. Kwa kuwa utafiti huu umechunguza lugha ya waathirika wa dawa za kulevya katika uga wa semantiki, mtafiti amependekeza tafiti zijazo ziangazie katika nyanja nyingine kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksi

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi wa jumla

Sura hii imetoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti ambayo ni “Maana Fiche ya Maneno yanayotumiwa na Waathirika wa Dawa za Kulevya”. Imeelezea usuli wa mada, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti.

1.2 Usuli wa mada

Dhana ya dawa za kulevya imejadiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwao wapo walioeleza kuwa dawa za kulevya ni kemikali ambazo ziingiapo mwilini huathiri ubongo wa mtumiaji na kumsababishia kuwa na matendo, hisia, fikra na muonekano tofauti na matarajio ya jamii ([www. Udsm.ac](http://www.Udsm.ac)). Matumizi ya dawa za kulevya ni janga la ulimwengu mzima. Tatizo linaendelea kukua kila kukicha, licha ya serikali na mashirika binafsi kupiga vita utengenezaji, usambazwaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Mwanzoni waathirika dawa za kulevya walikuwa zaidi ni vijana wa kiume lakini kufikia sasa, wanawake pia ni waathirika. Sio vijana tu hata watoto na wazee pia wamejiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya (Mohammed, 2017). Dawa hizi huingia mwilini kwa njia kuu tatu; njia ya kunywa au kula, njia ya kuvuta/kunusa na njia ya kudunga sindano.

Kato (2019), ameandika kuwa, jumla ya watu milioni 35 duniani kote wameathirika na dawa za kulevya na wanahitaji huduma za matibabu. Idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya imeongezeka, takwimu za mwaka 2017 zinaonesha kuwa, mwaka 2016 watumiaji wa dawa za kulevya walikuwa ni million 271. Ameongeza kuwa, waathirika zaidi wa janga hili ni watu wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 64 katika Afrika, Asia, Ulaya na Marekani ya kaskazini.

Mohammed (2017) ameandika kuwa, Dawa hizi hutumiwa na watu kati yamilioni 155 na 250 duniani. Idadi ya watu wanaotumia dawa za kulevya hivi sasa ni asilimia 30 zaidi ikilinganishwa na miaka 10 iliyopita. Watu wenye umri wa kati ya miaka 15-64, hutumia mihadarati Afrika, Asia, Ulaya na Amerika Kaskazini sambamba na matumizi ya bangi huko Amerika ya Kaskazini na Kusini, Asia pamoja na Afrika. Takwimu zilizofanywa Tanzania kwa mwaka 2015 zilionesha kuwa, wanaume wameendelea kuwa wahasika wakuu wa biashara ya dawa za kulevya pamoja na utumiaji wake, ingawa wanawake nao wanajihusisha na biashara hii, hasa wasichana japokuwa wanatumia kwa siri sana tofauti na wanaume.

Waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno ya kawaida lakini huwa na maana ya ndani iliyofichika kwa wanajamii na kutambulika na watumiaji wa dawa hizo tu. Vilevile, huunda maneno mapya yasiojulikana na wanajamii wengine. Yumkini hutumia maneno yenye maana fiche kwa lengo la kujitofautisha na makundi mengine au kwa sababu ya kutaka wasikamatwe na kutuhumiwa kwa kosa la utumiaji wa dawa za kulevya.

Samamba na kukamatwa kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya lakini bado baadhi ya watu wanaendelea kujihusisha na biashara hii haramu ya usafirishaji wa dawa za kulevya kama ambavyo Richard (2020) alivyoeleza kamatwa mtuhumiwa wa kike aliyekuwa akijaribu kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroini gramu 448.12 kutoka Dar es Salaam kwenda nchini India.

Sio Tanzania Bara tu, hata Visiwani Zanzibar tatizo hili la usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya bado lipo.

Naye Kabaleke (2020) akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, katika Mwanahalisi TV ameeleza kukamatwa kwa dawa za kulevya katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar. Kabaleke ameeleza kuwa, jeshi la polisi lilimkamata raia wa Marekani mwenye umri wa miaka 60 aliyekuwa na dawa za kulevya aina ya heroini kilo 4 akitaka kuziingiza Zanzibar. Baada ya kuhojiwa na polisi, mtuhumiwa huyo alikiri kosa hilo na kueleza alikozipata dawa hizo. Mtuhumiwa huyo alisema kuwa, dawa hizo aliuziwa na kijana mmoja mkaazi wa Magomeni Dar-es salaam. Alinunua dawa hizo kwa ajili ya kuziuzua Zanzibar na nyingine kuzisafirisha nchini Ubelgiji.

Pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na nchi mbalimbali duniani kupiga vita biashara haramu ya dawa za kulevya, bado nchi nyingi katika Bara la Afrika ikiwemo Zanzibar zinaendelea kupata changamoto. Changamoto kubwa ni zile zinazotokana na uzalishaji, utengenezaji na usafirishaji pamoja na matumizi haramu ya aina mbalimbali za dawa za kulevya; bangi, heroini, kokaini na mirungi. Mnamo mwaka 2009, Baraza la

Wawakilishi la Zanzibar lilipitisha Sheria Namba 9 ya 2009 ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya. Sheria hiyo ilianzisha Tume ya Taifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya ya Zanzibar (TTKKDKZ). Mfuko maalumu kwa ajili ya kuratibu na kudhibiti dawa za kulevya ulianzishwa. Lengo kuu ni kuratibu na kuishauri Serikali namna bora ya kudhibiti uingizwaji na utumiaji wa dawa za kulevya Zanzibar.

Pamoja na kuanzishwa tume hiyo na kuwepo kwa sheria iliyoweka adhabu kwa watakaokwenda kinyume na masharti ya sheria hii, bado tatizo la usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya linaendelea siku hadi siku katika visiwa vya Zanzibar. Vijana wengi wakiwemo wanafunzi wa skuli wanaendelea kujiingiza katika makundi ya watumiaji wa dawa za kulevya. Hatimae na wao kuathiriwa na dawa za kulevya.

Utumiaji wa maana fiche unaaminika kuwa ni sababu mojawapo inayokwamisha harakati za mapambano dhidi ya dawa hizo. Baadhi ya watoa taarifa wameeleza kwamba wanashindwa kutoa ushirikiano kwa mamlaka zinazohusika ili kuwakamata watumiaji, wauzaji na wasambazaji wa dawa hizo kwa sababu ya kutoelewa kile kinachozungumzwa na wauzaji au watumiaji wa dawa za kulevya. Mfano muuzaji na mnunuaji wa dawa za kulevya wanaweza wakawa wanapeana taarifa mbele ya wanajamii kuhusu kuwasili kwa dawa za kulevya na sehemu zinapopatikana. Wanajamii hushindwa kuelewa mazungumzo hayo kwa sababu waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno ya kawaida wakiwa na maana tofauti na ile inayofahamika na wanajamii. Endapo maana fiche hizo zitatambulika na wanajamii pamoja na taasisi zinazopambana na dawa za kulevya inatarajiwa kuwa

itaimarisha zaidi harakati za mapambano dhidi ya dawa hizo na hatimae kutokomeza matumizi ya dawa za kulevya Zanzibar.

1.3 Tatizo la utafiti

Watumiaji wa dawa za kulevya wanaonekana kutumia zaidi maneno yenye maana fiche yanayoeleweka na wao wenyewe tu. Maneno hayo huwatatiza watumiaji wengine wa lugha wasiokuwa katika kundi hilo. Inaaminika kuwa waathirika hawa wa dawa za kulevya hutumia maneno hayo kwa lengo la kuficha maana ili isiwe rahisi kukamatwa au kutuhumiwa kwa kosa la matumizi ya dawa za kulevya, hali hii huwatatiza wanajamii wengine. Kukosekana kwa Mawasiliano baina ya waathirika wa dawa za kulevya na jamii kwa upande mmoja, na waathirika na vyombo vya mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa upande mwingine kunakosababishwa na kutokueleweka kwa maana ya maneno ya waathirika wa dawa za kulevya ndio tatizo la utafiti huu. Mtafiti analenga kufichua maana hizo ili kuondoa tatizo hilo na kuziba pengo la kitaaluma liliopo.

1.4 Malengo ya utafiti

Katika kipengele hiki mtafiti amechambua malengo ya aina mbili ambayo ni lengo kuu na malengo mahsusi ya utafiti.

1.4.1 Lengo kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

1.4.2 Malengo mahsusi

Malengo mahsusi ya utafiti ni;

- a) Kubainisha maneno mahsusi yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.
- b) Kufafanua maana fiche za maneno mahsusi yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.
- c) Kujadili sababu za matumizi ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.
- d) Kutathmini athari za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

1.5 Maswali ya utafiti

- a) Ni maneno yepi mahsusi yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar?
- b) Ni zipi maana fiche za maneno mahsusi yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar?
- c) Ni zipi sababu za matumizi ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar?

Ni zipi athari za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar?

1.6 Umuhimu wa utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango mkubwa kwenye uga wa lughawiya katika kipengele cha semantiki na mofolojia. Aidha imezoeleka kwamba, wasomi wa sayansi ya afya na wanafasihi pekee ndio wanaoshughulika na utafiti kuhusiana na dawa za kulevya. Utafiti huu unakinzana na mawazo hayo kwa sababu utafiti huu wa kilughawiya, unalenga kutoa mchango mkubwa kwa taasisi zinazopambana na dawa za kulevya kwa kubaini maana fiche za maneno ya waathirika wa dawa za kulevya. Taasisi hizo zitazidi kuhamasika kufanya kazi kwa bidii pindi zitakapotambua kuwa, wasomi wa lughawiya nao wanathamini na kuunga mkono harakati zao. Vilevile, jamii itazielewa maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya na kushiriki katika kupambana na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Utafiti huu ni chachu ya kutoa fursa ya kufanya tafiti nyingine zinazohusiana na mada kama hii.

1.7 Mipaka ya utafiti

Utafiti huu umejikita kwenye taaluma ya lughawiya hasa katika kipengele cha semantiki. Hata hivyo, vipengele vya fonolojia, mofolojia na sintaksia vimehusishwa katika uchambuzi wa kisemantiki wa maneno yaliyochunguzwa. Utafiti huu kwa ujumla umeshughulikia maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Kijiografia utafiti huu umefanyika Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja katika Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi A na Wilaya ya Magharibi B.

1.8 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii imeeleza taarifa mbalimbali kuhusu mada ya utafiti. Sura imeanza kwa kutoa utangulizi wa sura nzima na kufuatiwa na usuli ambapo mtafiti ameelezea kwa kina kuhusiana na dhana ya dawa za kulevya, aina na njia ya utumiaji wa dawa za kulevya. Vilevile ameeleza hali ya tatizo la dawa za kulevya ulimwenguni, Afrika, Tanzania na Zanzibar. Pia akaeleza namna serikali inavyopiga vita uingizwaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Aidha, sura hii pamoja na mambo mengine imeeleza tatizo la utafiti na kuonesha pengo la utafiti. Sura ya pili inayofuata inazungumzia mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imejadili vipengele vikuu viwili; kazi tangulizi mbalimbali zinazohusiana na maana fiche na maana za dawa za kulevya na Kiunzi cha nadharia.

2.2 Kazi tangulizi

Katika hatua hii mtafiti amepitia maandiko mbalimbali kama vile tasnifu, vitabu, majarida na magazeti ili kubaini pengo la utafiti.

2.2.1 Mapitio ya jumla kuhusu maana za maneno

Wataalamu tafauti wamefasili neno maana, baadhi ya wataalamu hao ni; Habwe na Karanja (2004), na Matinde (2012), wote wanakubaliana kuwa, neno maana lina fahiwa nyingi, linaweza kudokeza sababu, kusudi, ishara, urejeleo, maelekezo, ufafanuzi, kufaa na ukweli. BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa maana ni dhana inayowakilishwa na neno au ni ufafanuzi wa kitu au jambo fulani. Wamitila (2016) wanaeleza kuwa, maana ni dhana ambayo inawakilishwa na neno au ni ufafanuzi wa jambo au kitu kinachofanya jambo au kitu chenyewe kieleweke. Tafiti hizo kwa ujumla zimehusiana na utafiti huu kwa sababu zote zinaelezea maana za maneno lakini zimetofautiana; wataalamu hao wameelezea dhana ya maana kwa ujumla ilhali utafiti huu umechunguza maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Maandishi haya yametoa mwanga kwa mtafiti

kufahamu dhana ya maana kwa ujumla kwa sababu ndio kipengele cha sarufi tunachokishughulikia.

Paneli la Kiswahili (2019) inaeleza kuwa, maana inaweza kuwa ya ndani au ya juu juu yaani maana iliyofichika au maana inayoeleweka haraka. Maana iliyofichika huhitaji kutafakari kwa kina ili kuitambua lakini maana iliyo wazi ni ile maana ya msingi ya neno na mara nyingi huwa ni ile iliyomo katika kamusi. Maana ya ndani huwa fiche na huhitaji hekima kuitambua. Maana ya juu huwa wazi; hurejelea vitu vinavyojulikana vizuri. Maelezo hayo yamemsaidia mtafiti kubaini aina ya maana anayoshughulikia (maana fiche). Ametanabahi kuwa, maana hiyo, inahitaji hekima zaidi katika kuitambua. Kwa sababu hiyo, ndipo akaona umuhimu wa kujikita moja kwa moja kwa watumiaji wa maneno yenyewe (waathirika wa dawa za kulevya) ili wamfafanulie maana hizo na hatimae kutimiza malengo ya utafiti.

Kotz na Paulmann (2011) wameelezwa kuwa, maana ya kihisi (emotive meaning) ni maana za kihisia ambazo hutokana na upotoshaji wa maana ya msingi (TY). Ni maana itokanayo na utumizi usio wa moja kwa moja ili kutoa maana. Maana ya kitu huwa ni ya mzunguko na fiche Maelezo hayo yamemsaidia mtafiti kutambua maana ya kihisi kuwa ni maana ambayo huwa na mzunguko katika kuitambua. Hivyo ili kuipata maana halisi ni lazima mzungumzaji au watumiaji wa maneno hayo wahusishwe. Hivyo mtafiti aliamua kwenda moja kwa moja uwandani na kukutana na waathirika wa dawa za kulevya ili kusikiliza maneno na kupata maana zake ambazo ni fiche zisizoweza kutambulika kwa wanajamii wengine.

Lehmann (1962) anaeleza kuwa maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi yake. Anaendelea kufafanua kwamba, kufahamu maana ya neno ni kuelewa matumizi yake sio tu kutafuta maana yake. Anaendelea kufafanua kwamba maana inayoibuliwa na neno au kauli hutokana na uwezo wake wa kutumika katika mawasiliano. Utafiti wa Lehmann umetoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwa sababu umemuwezesha mtafiti kuchambua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya wanapokuwa katika mawasiliano baina yao.

Crystal na Davy (1969) wanaeleza kuwa lugha inaweza kutumiwa kulingana na miktadha mbalimbali. Wanapambanua kuwa matumizi ya lugha katika miktadha na shughuli tofauti hurejelea rejista mbalimbali, matangazo katika redio na televisheni, ripoti katika magazeti ni baadhi ya zile ambazo wanaisimu hawa wameangazia sifa zao. Utafiti wa Crystal na Davy umehusiana na utafiti huu kwa sababu zote zimechunguza lugha kwa mujibu wa muktadha. Licha ya mfanano uliopo katika tafiti hizi, utafiti wa Crystal na Davy umelenga zaidi katika kuchunguza rejista ya matangazo katika vyombo vya habari ilhali utafiti huu umeshushulikia maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Inglis (1972) alifanya utafiti kuhusu lugha ya utangazaji. Alibainisha kuwa lugha hupata maana katika muktadha fulani na kwamba watu hupata maana za kipekee kwa kuhusisha maneno na tamaduni zinazozalisha maana hizo. Anasisitiza umuhimu wa kuzingatia muktadha, mazingira na tamaduni za hadhira inayokusudiwa ili kuweza kufikisha ujumbe

uliokusudiwa. Utafiti wa Inglis uliamsha hisia kwa mtafiti katika suala la muktadha jinsi linavyoibuwa maana mpya za maneno na kuamua kufanya utafiti wa maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Lengo likiwa ni kugundua maana mpya zinazoibuliwa na waathirika wa dawa za kulevya katika mazungumzo yao. Hata hivyo, utafiti wa Inglis unatofautiana na utafiti huu kwani haukulenga maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya katika mkoa wa Mjini Magharibi.

Falk (1973) anaeleza kwamba maana inatokana na matarajio ya washiriki katika mazungumzo. Hivyo, maana za maneno huangaza kusudio la msemaji na mwikio wa msikilizaji. Utafiti wa Falk umehusiana kwa namna fulani na utafiti huu kwa sababu zote zinaelezea maana kwa mujibu wa washiriki katika mazungumzo. Utafiti wa Falk umefafanua maana kwa mujibu wa wazungumzaji kwa ujumla na kuacha pengo la utafiti. Kwa upande wa utafiti huu mtafiti amechambua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Brown na Yule (1983) walifanya utafiti kuhusu uchambuzi wa matini. Matokeo ya utafiti wao yalionesha kuwa, usemi unaweza kuchambuliwa kwa kutilia uzito wa maana inayoibuliwa. Hali hii inaonesha kwamba, watumiaji wa lugha wakati mwingine humaanisha zaidi ya yale wayasemayo hasa wanapozingatia miktadha tofauti. Kwao usemi huweza kutumiwa kwa maana ya kimsingi au ya kawaida. Matumizi haya hulingana na maana dhanishi ambayo imefumwa katika utanzu wa semantiki. Kwa upande mwingine, kauli huweza kufasiliwa kiulinganishi pale inapotumiwa kwa njia maalumu. Utafiti wa

Brown na Yule umemsaidia mtafiti kutambua kuwa watumiaji wa lugha wakati mwingine humanisha zaidi ya yale wayasemayo hasa wanapozingatia miktadha tofauti. Hivyo ili kupata maana fiche za maneno inabidi kuwahusisha watumiaji wa lugha. Kwa mantiki hiyo, utafiti wa Brown na Yule umekuwa ni chachu kwa mtafiti wa utafiti huu kuchambua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Verstergaard na Shroder (1985) wametafiti lugha ya matangazo katika majarida. Walijadili mbinu za lugha zinazotumiwa na namna ya kufasili maana kwa kutumia nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo. Hata hivyo, utafiti wao haujalingana na utafiti huu kwa kuwa huu umechunguza maana fiche za maneno ya waathirika wa dawa za kulevya ili kuzifichua na kubainisha sababu za matumizi ya maana fiche na athari zake kwa jamiii. Aidha Habwe (1989) alifanyia utafiti vipashio vya sarufi amilifu mfumo katika usemi wa Kiswahili. Alibainisha nyenzo za kupatikana na kupitishwa kwa maana zinazotokana na mazungumzo ya kawaida miongoni mwa wazungumzaji wa Kimvita. Aliangalia maana iliyokusudiwa kutegemea muktadha na mahali. Utafiti huo umedhihirisha wazi kuwa, maana za maneno hupatikana kwa kuhusisha watumiaji na mahali. Kwa kuwa utafiti huo uliangazia kwa wazungumzaji wa kimvita, utafiti huu ni tofauti kwa vile umechunguza mazungumzo ya kawaida ya waathirika wa dawa za kulevya.

Aidha, Massamba (1987) alieleza athari za kisiasa katika maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania. Katika andiko lake, alieleza kuwa uibukaji wa maana za maneno na kauli

isiyozoeleka huweza kutokana na mazoea ya matumizi yake na maendeleo au mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali katika maisha. Utafiti wa Massamba pamoja na utafiti huu zimeelezea uibukaji wa maana mpya katika nyanja za maisha. Pamoja na hayo, Massamba ameshughulikia zaidi mabadiliko ya maana kutokana na maendeleo au mabadiliko yanayotokea katika nyakati za kisiasa lakini utafiti huu umetafiti maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Wendell (1992) akizungumzia uchanganuzi wa matini (ripoti), anaeleza kwamba uamilifu wa lugha hukamilika ndani ya matumizi yake katika muktadha maalumu. Maelezo haya yameshabihiana na malengo ya utafiti wetu yaliyonuia kubainisha maana fiche (mpya) ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Massamba (2016) anaeleza kuwa, maana ni kile ambacho neno au tungo huashiria kutokana ama na dhana, matumizi au kitajwa. Akaendelea kueleza kuwa, kuna aina mbalimbali za maana kama vile maana amilifu, ashirifu, jumuishi, leksika, halisi, dhamirifu, muktadha, sarufi na semantiki shawishi. Vilevile ameeleza kuwa, maana ya muktadha ni maana kwa mujibu wa mazingira ambamo neno fulani hujikuta ndani mwake. Kazi ya Massamba inahusiana na utafiti huu kwa kiwango fulani, kwa sababu yeye ametafiti kipengele cha semantiki pia kama ilivyo katika utafiti huu. Hata hivyo, Massamba amefasili dhana ya maana na kufafanua aina za maana ilhali utafiti huu umechambua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Ingawa hivyo, utafiti wa Massamba umetoa mwangaza katika uchambuzi wa aina za maana za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya.

O'Grady na wenzake (1997) wanafafanua mabadiliko ya kisemantiki yanayohusu kubadilika kwa maana za maneno katika lugha. Wamebainisha namna mbalimbali za mabadiliko kama vile upanuzi wa maana, kuhama kwa maana na ufifiishaji wa maana. Mawazo haya yanawiana kiasi na utafiti huu kwa kuwa yote yamejikita katika mabadiliko ya kisemantiki katika lugha. Utafiti huu umejitana zaidi na kuangazia katika kundi maalumu la wanajamii ambalo ni waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Hivyo, utafiti wa O'Grady umechangia kuimarisha utafiti huu katika uchambuzi wa maana fiche za maneno baada ya kutambua namna mabadiliko ya maana yanavyoweza kutokea katika lugha.

Habwe (1999) ametafiti hotuba za kisiasa nchini Kenya. Aligundua kuwa sitiari na maswali ya balagha hutumiwa mno katika hotuba za wanasiasa. Aligundua pia kuwa maana za hotuba huwa zaidi ya maana ya maneno yanayotumiwa na kwamba wanasiasa hugeza maana ili kutosheleza hali tofauti, matarajio na mahitaji ya hadhira yao. Utafiti wake ulimulika mshikamano, muwala na maana kipragmatiki. Kazi hiyo imedhihirisha kuwa wazungumzaji huweza kugeuza maana ili kukidhi mahitaji ya wazungumzaji. Utafiti wa Habwe umetimiza ari kwa mtafiti wa utafiti huu, kukusanya na kuchambua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya pamoja na kuweka wazi sababu na athari za matumizi ya maana fiche kwa jamii.

Suleiman (2015) alifanya utafiti kuhusu kiwango cha mabadiliko ya maneno ya Kipemba. Utafiti wake umebainisha kuwa, maneno ya Kipemba yapo katika mabadiliko na huko ndiko kukua kwa lahaja hiyo. Aligundua kuwa mabadiliko ya maneno hayo, kwa kiwango kikubwa huelekea kwenye maneno ya Kiswahili Sanifu. Vilevile amebainisha kuwa, maneno hubadilika kwa kiwango cha asilimia tafauti kwa mujibu wa muktadha. Alielezea sababu mbalimbali zilizosababisha mabadiliko hayo. Sababu kuu zikiwa ni kukua kwa sayansi na teknolojia, athari za kuhamahama kwa watu kwa ajili ya kutafuta maisha, maingiliano ya kindoa, mabadiliko ya kiutamaduni, sababu za kibiashara pamoja na sababu ya msimamo wa kidini. Utafiti wa Suleiman umehusiana na utafiti huu kwa sababu pia umeshughulikia namna maneno unavyoweza kubadilika au kubeba maana tafauti kwa mujibu wa watumiaji. Licha ya ufanano huo, utafiti wa Suleiman umetofautiana na utafiti huu kwa sababu yeye alifanya utafiti katika lahaja ya Kipemba lakini utafiti huu umeangalia maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Utafiti wa Suleiman umetoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwa sababu umemsaidia mtafiti kuchambua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya.

Rajab (2017) alieleza kuhusiana na mabadiliko ya maana za msamiati wa Kiswahili katika muktadha wa kisiasa. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa, wanasiasa hutumia misamiati tofauti katika hotuba kwa minajili ya kufikisha ujumbe na kuwasiliana na wafuasi wao. Mawasiliano hayo yamebainika kufikiwa kwa kutumia msamiati kutoka katika miktadha mingine ambayo husababisha msamiati huo kupanuka maana, kufinyika

maana, usogezi na uimarikaji wa maana. Ni dhahiri kuwa, maana inayoibuliwa katika muktadha huo wa kisiasa huwa si ya kudumu dumifu kwani maana hiyo ni kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wakati ule tu. Ameendelea kueleza kuwa, jamii inatakiwa kuelewa tofauti za fikra kuhusu ukubalifu wa maana mpya za msamiati katika muktadha wa kisiasa. Hii ni kwa sababu, uibukaji wa maana mpya ya msamiati mara nyingi huathiri maisha binafsi ya mtu. Utafiti wa Rajab umehusiana na utafiti huu kwa sababu tafiti hizi zote zimelenga kuangalia kipengele cha semantiki katika muktadha maalumu. Hata hivyo, utafiti wa Rajab umetafautiana na utafiti huu kwa sababu yeye ameshughulikia namna maana zinavyoweza kubadilika katika muktadha wa kisiasa lakini utafiti huu umeshughulikia maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Mapitio yote hayo yaliyochambuliwa hapo juu, yamemsaidia mtafiti kutambua dhana ya maana kwa ujumla, aina za maana na namna maana inavyoweza kufasiliwa. Kwakuwa tafiti hizo zimeeleza dhana ya maana na aina zake kwa ujumla. Mtafiti ameona kuna pengo la utafiti kwa sababu hakuna utafiti wowote ulioshughulikia maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Sehemu hiyo imebaki na pengo la kitaaluma ambalo utafiti huu umelenga kuliziba. Hivyo, utafiti huu umeangalia maana fiche za maneno yanayotumiwa na kundi moja tu la wanajamii ambalo ni waathirika wa dawa za kulevya.

2.2.2 Mapitio kuhusu dhana ya dawa za kulevya

Tanzanian German Programme to Support Health (2007) wameeleza maana ya dawa za kulevya, aina zake na athari zake kwa watumiaji. Kwa upande wa athari za dawa za

kulevya, wameeleza kuwa, huathiri ubongo wa mtumiaji. Katika maelezo yao, wamebainisha athari za muda mrefu na zile za muda mfupi zinazotokana na utumiaji wa dawa hizo. Wamefafanua kuwa, Dawa za kulevya hutoka nchi mbalimbali duniani, kwa mfano kokaini inatoka Amerika ya Kusini, heroini hutoka Bara la Asia, India, Pakistan na Burma. Dawa zinazotengenezwa viwandani kama mandrax zinatoka nchi nyingi duniani, ikiwemo Tanzania. Bangi na mirungi hulimwa pia Tanzania.

Kutokana na maelezo haya, mtafiti ameweza kutambua aina za dawa za kulevya na kutambua wapi zinakotoka na vipi zinafika Tanzania. Hali hii imemfanya mtafiti kutambua mtandao wa dawa za kulevya nje na ndani ya Tanzania. Maelezo ya TGPSH yamehusiana na utafiti huu kwa sababu zote zimejiegemeza kwa waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Pamoja na uhusiano uliopo, mtafiti amebaini pengo la utafiti; TGPSH wametafiti zaidi katika uga wa sayansi ya afya lakini utafiti huu ni wa kilughawiya na umetafiti maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya (sayansi ya lugha).

Ame (2013) katika makala yake, ameeleza kuwa mke wa Rais wa Zanzibar (wakati huo) mama Mwanamwema Shein, alitembelea katika nyumba za kubadilisha tabia (soba), na kuwataka waathirika wa dawa za kulevya kubadili mwenendo wao mzima wa maisha ili waweze kuachana na matumizi ya dawa hizo. Vilevile aliwataka waathirika hao wawashauri vijana wengine ambao bado wanatumia dawa hizo kuacha na kujiunga katika nyumba hizo. Nyumba hizo ni Bububu, Nyarugusu, Zanzibar Youth Forum, Tawabina,

Women soba, Bombay soba, Betroit soba kwa Unguja, Chakechake soba na Wete soba kwa Pemba.

Makala ya Ame imeshabihiana na utafiti huu kwa kuwa zimeangalia kundi la aina moja la watoa taarifa ambalo ni waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Kwa upande mwingine, utafiti wa Ame umeelezea kuhusu ziara ya Bi Mwanamwema Shein, nasaha zake kwa waathirika wa dawa za kulevya na kutaja nyumba za kurekebishia tabia bila kugusia katika uga wa lughawiya. Kwa kuwa uga wa lughawiya haukugusiwa, mtafiti ameona ipo haja ya kupiga hatua zaidi kwa kutafiti maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Makala hii imemsaidia mtafiti kutambua idadi ya nyumba za kurekebishia tabia za waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar na kutambua juhudi za viongozi wa serikali katika kupambana na dawa za kulevya. Katika nyumba hizo mtafiti ameweza kuwapata watoa taarifa wa aina mbili; waathirika wa dawa za kulevya na wahudumu. Hivyo kupitia taasisi hizo mtafiti ameweza kukusanya data zinazohusiana na malengo ya utafiti.

John (2017), ameeleza kukamatwa kwa watu ishirini (20) kwa msaada wa mbwa wa polisi mkoani Singida wakituhumiwa kujihusisha na usambazaji wa dawa za kulevya. Watu hao walikamatwa baada ya jeshi la polisi kutumia mbwa kukagua mabasi yanayoingia na kutoka mkoani hapo. Misokoto 7000 ya bangi, unga aina ya heroini na Mirungi ilikamatwa. Kamanda wa polisi wa mkoa huo Bi Debora alisema wauzaji na watumiaji wamekuwa wakibuni njia mpya kila siku kwa ajili ya kufanikisha shughuli zao. Makala ya John

inadhihirisha kuwa; wengi wa walioathirika nchini Tanzania ni watumiaji wa bangi, mirungi na heroini ambao ni moja kati ya watoa taarifa wa utafiti huu.

Mayala (2019) amefafanua aina na athari za dawa za kulevya kwa mtumiaji, ameeleza kwamba dawa za kulevya humfanya mtumiaji kuwa na hisia na matendo tafauti na matarajio ya jamii, kwa mfano mtu huwa mpole kupita kiasi au mkali au mchangamfu na mwingine hucheka sana. Mtafiti anakubaliana na mawazo ya Mayala na yamemsaidia kutambua tabia za kundi moja la watoa taarifa wake ambalo ni kundi la waathirika wa dawa za kulevya na kuandaa njia madhubuti za kukabiliana na watoa taarifa wake wakati wa ukusanyaji wa data. Kinyume na maelezo ya Mayala ambayo yameangazia aina na athari za dawa za kulevya kwa mtumiaji, mtafiti wa utafiti huu amechambua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya mifano kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi.

Shine (2015), aliandika makala iliyozungumzia aina za dawa za kulevya. Alibainisha dawa au vilevi ambavyo vinapotumiwa hubadilisha mfumo wa mwili na akili ya mtumiaji. Hudhoofisha mwili na kupata madhara ya kiakili na hatimaye huweza kusababisha kifo. Pia, aligundua sababu za vijana kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya; kufuata mkumbo wa marafiki na watu waliowazunguka katika jamii, kuukimbia ukweli wa tatizo linalomkabili mathalani umeachwa na mke au mpenzi, umasikini na ugonjwa. Pia baadhi ya vijana hutumia dawa za kulevya ili kuonja ladha ya dawa hizo au kutaka kujua nini atahisi baada ya kutumia. Wapo pia wanaotumia dawa za kulevya bila ya kujua kwanini

wanatumia. Katika kundi hili mathalani mpenzi wako ni mtumiaji wa dawa za kulevya, kidogo kidogo huweza kushawishika na kuanza kutumia pia. Makala hii imetuonesha baadhi ya sababu za matumizi ya dawa za kulevya jambo ambalo limemsukuma mtafiti kuchunguza maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya, sababu za matumizi ya maana fiche pamoja na athari zake kwa jamii ya waZanzibari.

2.3 Kiunzi cha nadharia

Verschurch (2005) ameeleza kwamba nadharia ni njia ambazo husaidia katika utoaji maoni au mawazo ambayo yatamfanya mtafiti kupata maoni ya kazi yake. Sengo (2009) ameeleza kuwa nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, muongozo mkuu wa mtu au watu (jamii) pahala fulani, wakati fulani na ni muongozo wa kufuata wakati wa kuchambua kazi za utafiti. Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili; Nadharia kidhi ya mawasiliano na nadharia ya maana ni matumizi.

2.3.1 Nadharia kidhi ya mawasiliano (NkM)

Nadharia hii imeasisiwa na Howard Giles mwaka 1973. Katika utafiti wake (Giles) ulibaini kuwepo kwa mabadiliko ya kimatamshi na kimsamiati kwa wazungumzaji walio wengi na alipenda kufahamu kiini cha tatizo hilo. Lengo kuu la nadharia hii ni kuonesha sababu za kubadili mtindo wa kimatamshi na kimsamiati katika kufanya mawasiliano katika jamii inayohusika.

Inasadikiwa kwamba, wanaadamu katika maisha yao hujaribu kuiga aina fulani ya matamshi kutoka kwa mtu mwingine ili waweze kukidhi kiu yao ya kufanya mawasiliano

baina yao na mtu mwingine. Yumkini wanadamu hao (hufanya wigo) huiga maneno au vipengele vyengine vya lugha kutoka kwa mtu mwingine anayefanya naye mazungumzo kwa kujielewa au kwa kutojielewa.

Tukitolea mfano mzungumzaji mmoja hufanya mtindo wa wigo katika matamshi ya lugha ya mzungumzaji mwingine na kukidhi lafudhi kwa lugha ya mzungumzaji mwingine. Giles anaeleza; miongoni mwa sababu kuu za kubadili mtindo wa kimatamshi ni kuashiria uhusiano na mafungamano ya watu wa jamii nyengine. Ndio maana hutokea hili au hujulikana hili na watu waliojilinganisha katika mahusiano yao. Katika nadharia hii, mawasiliano ya kiisimu hugawika katika makundi makuu mawili; mawasiliano wima na mawasiliano yasiyo wima. Mawasiliano wima ya kiisimu hujitokeza miongoni mwa wazungumzaji, mmoja wao anapokuwa ni mweledi zaidi wa lugha, hivyo yule ambaye si mweledi hujaribu kufanya wigo ili kumfikia huyu aliye mweledi zaidi wa lugha.

Nayo mawasiliano yasiyo wima mara nyingi hujitokeza pale ambapo mzungumzaji fulani anapozungumza na watu wa rika la vijana na ikabidi ajilazimishe kuimarisha lugha ili aweze kukidhi haja ya kufanya mawasiliano yanayopendeza zaidi baina yao. Hivyo, mkazo wa lugha hujitokeza katika muktadha wa utambulisho. Nadharia kidhi ya mawasiliano (NkM) inatambua kuwa;


- i. Historia za watu na uzoefu wao kupitia matamshi yatokanayo na mawasiliano yao pamoja na tabia zao, hutoa mwanya wa kuwepo ufahamu wa kimatamshi na tabia fulani ndani ya mazungumzo yao.

- ii. Ndani ya jamii mawasiliano huathiriwa na mazungumzo ambayo hutoa tafsiri na kuuhukumu ujumbe uliobebwa katika mazungumzo hayo.
- iii. Kwa muktadha huo mawasiliano huweza kugeuka kutokana na kaida na hali ya jamii inayohusika.

Nadharia hii imetosheleza mahitaji ya utafiti huu kwasababu inayo mihimili ya kutumika katika utafiti huu kwa kuwa, maeneo yote yanayohusisha mawasiliano yanaweza kufanyiwa kazi vizuri na nadharia hii.

Kwa vile dhamira kuu ya nadharia hii ni kuonesha mitindo ya maneno katika mawasiliano, sababu za kubadili mtindo wa matamshi na maumbo ya maneno ndani ya mawasiliano ya jamii fulani pamoja na kuangalia athari zake ndani ya jamii hiyo, mtafiti ameona ni muhimu kuitumia nadharia hii. NkM inaendana na kulingana na utafiti huu kwasababu imemsaidia mtafiti kuchunguza maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya kama ambavyo lengo la kwanza la utafiti linavyoelekeza, kubaini sababu zinazowasukuma waathirika wa dawa za kulevya kutumia maana fiche ikiwa ni mahitaji ya lengo la tatu pamoja na kuchunguza athari za maneno hayo ambalo ndiyo lengo la nne la utafiti. Mchoro ufuaao unaonesha namna NkM ilivyosaidia katika kutafiti maneno, sababu na athari za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar

Mchoro Na. 2.1 Nadharia kidhi ya mawasiliano



Chanzo: Mtafiti

2.3.2 Nadharia ya maana ni matumizi (NmM)

Nadharia hii iliasisiwa na mwanafalsafa Ludwig Wittgenstein (1963). Nadharia hii iliibuka ili kutatua upungufu uliojitokeza katika nadharia za maana zilizotangulia. Mfano wa nadharia hizo ni nadharia ya urejeleo, nadharia ya uelekezi, nadharia ya dhana au taswira, nadharia ya kichocheo na nadharia ya masharti ya ukweli.


Ludwig katika kitabu chake anaeleza kuwa, ni kosa kubwa kuangalia maana ya neno kama kitu au umbile kamili. Hivyo, alipendekeza kuwa maana ya neno iangaliwe kwa kuzingatia muktadha wa neno au msembo jinsi ulivyotumika. Hivyo maana ya neno au msembo ni matokeo au athari inayopatikana. Mwanafalsafa huyo, akaendelea kueleza kuwa; neno moja huweza kuwa na maana nyingi kutokana na matumizi yake katika tungo. Mwanafalsafa huyu, ameeleza mihimili ya nadharia hii ambayo ndiyo iliyomuongoza mtafiti katika Utafiti huu. Kuna mhimili mkuu na mihimili midogo midogo ya nadharia ya maana ni matumizi.

Mhimili mkuu wa nadharia hii unaeleza kwamba maana haipatikani kwa kuangalia neno pekee bali hupatikana kwa kuangalia namna gani watu au jamii wanavyolitumia neno hilo katika miktadha tofauti (Mdee, 1998).

Mihimili midogo midogo ya nadharia hii inaeleza kuwa hatuwezi kupata maana ya neno bila kuangalia lilitumika namna gani, wapi, watu wa jinsia gani, na umri gani katika jamii inayohusika. Kupitia nadharia hii, mtafiti amefanikiwa kukusanya maneno na kuchambua maana fiche zitokanazo na maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya kama

ambavyo lengo la pili la utafiti linavyoeleza. Hivyo, nadharia hii imetumika katika kutimiza lengo moja la utafiti huu kama inavyooneshwa katika mchoro ufuatao:


Mchoro Na. 2.2 Nadharia ya maana ni matumizi



Chanzo: Mtafiti

Hivyo, nadharia kidhi ya mawasiliano na nadharia ya maana ni matumizi zimeweza kusaidia kukamilisha uchunguzi wa utafiti huu kwa malengo yote manne. Mchoro ufuatao unaonesha namna nadharia hizi mbili zilivyomsaidia mtafiti kukamilisha malengo ya utafiti.

Mchoro Na. 2.3 Nadharia zilivyotumika katika utafiti



Chanzo: Mtafiti

2.3 Hitimisho

Sura hii imeonesha kazi tangulizi za wataalamu tofauti ambazo mtafiti alizipitia zinazohusiana na dawa za kulevya pamoja na maana za msamiati. Aidha, pengo la utafiti

lilioneshwa katika kazi hizo. Mwisho, sura hii imeonesha mkabala wa kinadharia ambao umeongoza utafiti huu na imefafanuliwa na kubainishwa sababu za kutumia nadharia hizo katika kulifikia lengo kuu la utafiti kama ilivyotarajiwa. Katika sura ya tatu inayofuata, mtafiti amefafanua mbinu za utafiti pamoja na vifaa vya utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti zinafafanuliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti ziko katika makundi makubwa mawili, ambayo ni mbinu za kukusanyia data na mbinu za kuchanganulia data. Data za utafiti huu zimekusanywa na kuchambuliwa kulingana na utaratibu uliopangwa na mtafiti. Katika sura hii, mtafiti ameelezea mbinu mbalimbali ambazo zimetumika kuendesha utafiti huu. Ili kufanikisha hilo, vipengele vifuatavyo vimeangaliwa kwa undani; mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa Sampuli, mbinu za kukusanyia data, vifaa vya kukusanyia data, mbinu za uchanganuzi wa data, uthabiti na kuaminika kwa data, miiko ya utafiti.

3.2 Mkabala wa utafiti

Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani kutoka kwa makundi mbalimbali ya watoa taarifa kama itakavyooneshwa katika kipengele cha usampulishaji. Aidha baada ya ukusanyaji wa data, mtafiti alizichambua data hizo kwa kutumia mkabala usio wa kiidadi kwa kiasi kikubwa na kwa kiasi kidogo mkabala wa kiidadi umetumika kuweka majadwali ili kubainisha matokeo ya utafiti.

3.3 Eneo la utafiti

Utafiti huu umefanyika Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi A na Wilaya ya Magharibi B. Katika Wilaya ya Mjini Magharibi

Unguja, mtafiti ametafiti katika maeneo ya Mwembeladu, Mpendae na Miembeni. Kwa upande wa Wilaya ya Magharibi A, mtafiti amefanya utafiti wake katika eneo la Bububu, Kianga na Bumbwisudi na Wilaya ya Magharibi B, maeneo ya Kisauni, Mwanakwerekwe na Fuoni yalitafitiwa. Mtafiti ameteua maeneo hayo kwa sababu inaaminika kuwa ndio maeneo yenye idadi kubwa ya waathirika wa dawa za kulevya. Vilevile katika Wilaya hizi nyumba za kurekebishia tabia za waathirika (soba) na taasisi za kupambana na dawa za kulevya zinapatikana.

3.4 Uteuzi wa sampuli

Mtafiti wa utafiti huu amekigawa kipengele hiki cha uteuzi wa sampuli katika makundi mawili; sampuli ya utafiti na mchakato wa usampulishaji kama unavyofafanuliwa hapa chini.

3.4.1 Sampuli ya utafiti

Kothari (2004) anafafanua sampuli kuwa ni kundi dogo la watoa taarifa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambapo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake. Hivyo, sampuli ni sehemu ya watoa taarifa inayowakilisha idadi kubwa ya watoa taarifa. Utafiti huu umetumia sampuli kutoka makundi ya aina tano. Sampuli ya kwanza ni waathirika wa dawa za kulevya. Katika sampuli hii mtafiti ametumia mbinu ya majadala wa kundi lengwa na ushuhudiaji. Kupitia mbinu hizo mtafiti amebaini maneno yenye maana fiche pamoja na maana zake zilizofichika ambazo hutumiwa na wathirika wa dawa za kulevya, sababu za utumiaji wa maana fiche pia amebaini athari za maana fiche kwa jamii. Katika kundi hili mtafiti amewatafiti jumla ya waathirika arobaini (40) kati ya mia moja na ishirini na

tisa (129) ambao walipatikana katika maeneo ya aina tatu; nyumba za kurekebisha tabia za waathirika wa dawa za kulevya, kliniki za waathirika wa dawa za kulevya na katika maskani za waathirika wa dawa za kulevya. Watoa taarifa watano walipatikana kutoka katika kila nyumba kati ya nyumba tano za kurekebisha tabia zilizopo Kwa binti Imran, Bububu Kijichi, Fuoni, Kisauni na Mpendae. Jumla ya sampuli ya waathirika wanaoishi katika nyumba za kurekebisha tabia ni ishirini na tano (25) kati ya waathirika hamsini (50).

Katika kliniki za waathirika wa dawa za kulevya, waathirika kumi (10) kati ya thelathini na sita (36) wa dawa za kulevya walipatikana kutoka katika kliniki mbili za waathirika wa dawa za kulevya (Mati kliniki iliyopo Kidongo Chekundu na Kituo Cha Afya cha Mwembeladu kitengo cha huduma na matibabu). Kila kliniki wametafitiwa waathirika watano. Vile vile, mtafiti ametembelea maskani tano za waathirika wa dawa za kulevya na kushuhudia maneno mbalimbali yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Pia mtafiti alifanya usaili kwa muathirika mmoja kwa kila maskani. Hivyo kupatikana kwa sampuli ya waathirika watano (5) kati ya waathirika arobaini (40) na kukamilisha sampuli kuu ya waathirika arobaini wa dawa za kulevya.

Sampuli ya pili ni wahudumu wa taasisi sita zinazopambana na dawa za kulevya ambao walifanyiwa usaili. Hapa mtafiti amehusisha sampuli ya wahudumu kumi (10) kati ya ishirini na tatu (23) ambao walieleza sababu na athari za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Katika sampuli hii,

wahudumu sita wamesailiwa kutoka katika nyumba tatu; wawili kutoka katika kila nyumba ya kurekebisha tabia. Wanne (4) kati ya wahudumu nane (8) kutoka katika kliniki mbili za waathirika wa dawa za kulevya ambapo kila kliniki wametafitiwa wahudumu wawili. Sampuli ya tatu ni askari watatu (3) kati ya ishirini na moja (21) wa kitengo cha kupambana na dawa za kulevya Zanzibar ambao wamefanyiwa usaili katika vituo vyao vya kazi (kituo cha polisi Madema, kituo cha polisi Bububu, kituo cha polisi Fuoni). Watoa taarifa hao wameeleza sababu na athari za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya.

Sampuli ya nne ni walimu; mtafiti amekusanya taarifa kwa kuwasaili walimu kumi 10 kati ya walimu tisini na tatu (93), wawili kutoka kila skuli kati ya skuli tano walisailiwa. Skuli hizo ni skuli ya Sekondari ya Bububu, Skuli ya Mwenge, Skuli ya Kianga, Skuli ya Kidongo Chekundu na Skuli ya Fuoni. Watoa taarifa hao wameeleza sababu na athari za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Sampuli ya mwisho ni wazazi/walezi; mtafiti amewasaili wazazi/walezi kumi (10) kwa kupitia majina ya wanafunzi wanaotuhumiwa kujihusisha na makudi ya watumiaji wa dawa za kulevya katika skuli teule. Wazazi/walezi wawili kutoka katika kila skuli walisailiwa na kueleza sababu na athari za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Hivyo utafiti huu umetumia sampuli tano na jumla ya watoa taarifa sabini na tatu (73). Watoa taarifa hawa walichaguliwa kwa sababu ndio waliokuwa na uwezo wa kutoa taarifa zinazohitajika katika utafiti huu.

Jadweli Na. 3.1: Ufafanuzi wa mgawanyo wa sampuli

Na	Sampuli	Eneo la Utafiti	Idadi ya Maeneo	Watoa taarifa	Jumla	%
1	Waathirika wa dawa za kulevya	a) Nyumba za kurekebishia tabia za waathirika wa dawa za kulevya.	5	5	25	34.2
		b) Kliniki za waathirika wa dawa za kulevya	2	5	10	13.5
		c) Maskani za waathirika wa dawa za kulevya	5	1	5	6.9
2.	Wahudumu	a) Nyumba za kurekebishia tabia	3	2	6	8.2
		b) Kliniki za waathirika wa dawa za kulevya	2	2	4	5.5
3	Askari wa kupambana na dawa za kulevya	Kitengo cha mapambano dhidi ya dawa za kulevya	3	1	3	4.1
4	Walimu	Skuli teule	5	2	10	13.7
5	Wazazi/Walezi	Skuli teule	5	2	10	13.7
JUMLA					73	100

3.4.2 Usampulishaji

Kwa mujibu wa Sign (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watoa taarifa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Sampuli huchaguliwa kwa njia mbalimbali kama vile usampulishaji nasibu na usiyonasibu. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji nasibu. Ponera (2019) anauelezea usampulishaji nasibu kuwa ni mchakato wa kuteua sampuli ambao unatoa fursa sawa ya kutafitiwa kwa kila kitafitiwa kilichomo kwenye jumuiya ya utafiti. Ili kufanikisha

malengo ya utafiti, mtafiti ametumia mbinu mbalimbali katika mchakato wa usampulishaji nasibu kama vile kutumia mbinu ya kutabakisha.

Mtafiti ametumia mbinu ya kutabakisha kwa kuwagawa watoa taarifa katika makundi matano kama yalivyokwishaelezwa. Makundi hayo yamegawanywa kwa mujibu wa kazi, sifa, hadhi na tabia za watoa taarifa. Mtafiti amewapata watoa taarifa kwa kutembelea katika kliniki za waathirika wa dawa za kulevya, nyumba za kurekebishia tabia za waathirika wa dawa za kulevya, maskani za waathirika wa dawa za kulevya, askari wa kitengo cha kupambana na dawa za kulevya, skuli zilizoteuliwa ili kukutana na walimu na pia kuwapata wazazi/walezi wa wanafunzi wa skuli hizo.

Kwa kuwa watoa taarifa wote wana fursa sawa, mtafiti ameipata sampuli lengwa kwa kutumia mbinu ya kubahatisha. Sampuli ya waathirika wa dawa za kulevya waliopo katika nyumba za kurekebishia tabia, wahudumu wa waathirika wa dawa za kulevya, askari wa kitengo cha kupambana na dawa za kulevya, walimu na wazazi wa wanafunzi wamepatikana kwa kubahatisha kwasababu mtafiti alimuomba mkuu wa kituo/kitengo teule amkutanishe na watoa taarifa wowote ambao wanaopatikana kwa wakati huo. Hivyo kupatikana kwa wamtoa taarifa hakukufanywa kwa kulengwa au kusudio lolote la mtafiti.

Kwa upande mwingine mtafiti amemtumia mtafiti msaidizi katika ukusanyaji wa data hasa zile za kutoka kwa waathirika wa dawa za kulevya maskanini. Katika eneo hili mbinu ya ushuhudiaji ilitumika. Ushuhudiaji ulifanyika kwa kubahatisha. Kila muathirika aliyepatikana aliweza kutafitiwa. Kwa hivyo, inadhihirika wazi kuwa mbinu ya

kutabakisha na kubahatisha zote zimetoa fursa kwa kila mwanajumuiya kuweza kuwemo katika sampuli inayohitajika; na kwamba kupatikana kwa mtoa taarifa fulani hakukufanywa kwa kulengwa au kusudio lolote la mtafiti.

3.5 Mbinu za kukusanyia data

Kothari (2004) ameeleza kuwa, mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Data za utafiti huu zimekusanywa uwandani kwa kutumia mbinu tatu; mbinu ya mijadala ya kundi lengwa, mbinu ya usaili na mbinu ya ushuhudiaji. Mbinu hizi za ukusanyaji wa data zimemuwezesha mtafiti kukusanya taarifa za kutosha katika utafiti wake kama zinavyoelezewa hapo chini.

3.5.1 Mbinu ya usaili

Mtafiti ameteua mbinu hii kwa sababu alikusudia kutoa fursa kwa mtoa taarifa kujieleza kwa upana zaidi. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti amefanikiwa kupata maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya, maana fiche za maneno hayo, sababu za matumizi ya maana fiche na athari za matumizi ya maana fiche kwa jamii ya Wazanzibari. Vilevile kwa kutumia mbinu hii, mtafiti amefanikiwa kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi, kwa sababu watoa taarifa waliweza kuuliza maswali ya ziada. Aidha, mbinu hii imetoa fursa kwa mtafiti kuwasiliana na watoa taarifa wake kwa njia ya kimtandao kama vile simu na kompyuta. Usaili ulitumika kwa askari wa kitengo cha mapambano dhidi ya dawa za kulevya, walimu, wazazi au walezi pamoja na wahudumu wa waathirika wa dawa za kulevya katika kliniki na katika nyumba za kurekebishia tabia.

3.5.2 Mjadala wa kundi lengwa

Hii ni njia ya kukusanya data inayohusisha mazungumzo baina ya mtafiti na watoa taarifa wakiwa katika vikundi juu ya mambo anayotaka kuyapata. Katika mbinu hii mtafiti aliwagawa watoa taarifa katika makundi ya watu sita na kujadiliana nao ili kupata taarifa za utafiti huu. Mtafiti aliteua mbinu hii kwa sababu baadhi ya watoa taarifa huwa hawapo huru kuzungumza wakiwa peke yao, hivyo njia hii imekuwa mwafaka kwao. Mbinu hii imetumika kwa waathirika wa dawa za kulevya waliopo katika nyumba za kurekebisha tabia za waathirika wa dawa za kulevya na katika kliniki za waathirika wa dawa za kulevya.

3.5.3 Mbinu ya ushuhudiaji

Nunan (1992) anadai kuwa ili kugundua tabia fulani, mtafiti hana budi kuichunguza katika mazingira ya utokeaji wake. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kwa kwenda katika maeneo halisi ya utafiti na kufuatilia kwa ukaribu au ana kwa ana. Mbinu hii ilitumika zaidi katika maskani za waathirika wa dawa za kulevya. Katika kundi hili, mtafiti hakuwa peke yake aliambatana na mtafiti msaidizi ambaye aliwahi kutumia dawa za kulevya pia ni mtu mwenye ukaribu mkubwa na kundi hilo la waathirika wa dawa za kulevya. Hii ni kwa sababu ya kuwaondoa hofu watoa taarifa na hatimae kufanikisha malengo ya utafiti.

Mbinu hii ilitoa fursa kwa mtafiti kushuhudia katika tukio au jambo na kuweza kukusanya taarifa kwa njia ya ugunduzi. Mtafiti alishuhudia kwa macho na kusikiliza mazungumzo ya waathirika ambayo ndani yake aliweza kupata maneno yenye maana fiche.

3.6 Vifaa vya kukusanyia data

Mtafiti ametumia vifaa vifuatavyo katika utafiti wake:

3.6.1 Daftari na kalamu

Mtafiti ametumia daftari na kalamu katika kunukuu na kuhifadhi baadhi ya data za utafiti huu kwa ajili ya kumbukumbu za baadaye wakati wa uchambuzi wa data hizo. Kifaa hiki kilimrahisishia sana mtafiti wakati wa mchakato wa uchambuzi wa data.

3.6.2 Kinasa sauti

Kifaa hiki kimetumika katika kunasa na kurekodi sauti wakati wa usaili, ushuhudiaji na mijadala ya kundi lengwa. Baadae wakati wa uchambuzi wa data, mtafiti alirejelea sauti zilizorekodiwa na kumpatia mazungumzo halisi ya watoa taarifa wake.

3.6.3 Kompyuta

Imetumika katika kutafutia kazi tangulizi na taarifa mbalimbali zinazohusiana na utafiti huu kupitia mtandao. Pia kompyuta imetumika kuhifadhi taarifa na kuandaa ripoti ya utafiti. Aidha, kompyuta imetumika kama sehemu ya maktaba tembezi.

3.6.4 Flashi

Kifaa hiki kimetumika kusafirishia data mbalimbali katika mchakato mzima wa utafiti. Kifaa hiki kimesaidia sana kurahisisha mchakato wa uchambuzi na uchapishaji wa tasnifu.

3.6.5 Muongozo wa usaili

Muongozo wa usaili umetumika wakati wa kukusanya data kwa wahudumu wa waathirika wa dawa za kulevya, askari, walimu, wazazi au walezi kwa ajili ya utafiti huu unaohusu maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Muongozo wa usaili ulimuongoza mtafiti kubaki katika malengo yake na kutotoka nje wakati wa mahojiano.

3.6.6 Muongozo wa mjadala wa kundi lengwa

Katika utafiti huu kifaa hiki kimetumika kwa ajili ya maswali ya kumwongoza mtafiti wakati wa kuwatafiti waathirika wa dawa za kulevya waliopo katika nyumba za kurekebisha tabia za waathirika wa dawa za kulevya na kliniki za waathirika wa dawa za kulevya. Kilikuwa kifaa muhimu sana kwa ajili ya kufanikisha kazi ya ukusanyaji data kutoka kwa watoa taarifa walioainishwa.

3.7 Mbinu za uchanganuzi wa data

Kwa mujibu wa Walliman (2011) amefafanua kuwa, data huchanganuliwa katika mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kiidadi na mkabala usio wa kiidadi. Mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo hutumia nambari kurikodi taarifa na huchanganuliwa kwa kutumia mbinu za kitakwimu. Naye Enon (1998) ameeleza kuwa, mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Mtafiti katika utafiti huu, amechambua data kwa kutumia mkabala usio wa kiidadi kwa kubainisha maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya,

kuchambua maana fiche za maneno hayo kwa mujibu wa watumiaji wa dawa za kulevya. Mtafiti pia ameelezea sababu za matumizi ya maneno yenye maana fiche pamoja na athari zake kwa jamii. Ilipobidi mtafiti alitumia majadwali kubainisha matokeo ya utafiti wake. NmM na NkM ndizo zilizomuongoza mtafiti katika uchambuzi wa data kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu yanavyoelekeza.

3.8 Uthabiti na kuaminika kwa data

Sehemu hii mtafiti ameigawa katika vipengele viwili; uthabiti wa mbinu za kukusanyia data na kuaminika kwa data.

3.8.1 Uthabiti wa mbinu za kukusanyia data

Kothari (2004) anafafanua kwamba uthabiti ni kiwango ambacho mbinu za utafiti zinapima kile kilichotakiwa kupimwa na mbinu hiyo. Naye Sign (2007) anasisitiza kuwa dhana au mbinu zote zilizotayarishwa kwa ajili ya kufanyia utafiti lazima zipimwe ili kuona kama zinafaa katika mazingira halisi yaliyokusudiwa. Kwa msingi huo mtafiti aliupima muongozo wa usaili aliouandaa kwa watu ambao sio walengwa wa utafiti huu lakini wana sifa zinazofanana na watoa taarifa wake. Kabla ya data za utafiti kukusanywa mtafiti aliwasaili vijana ambao hukaa maskani kwa ajili ya mazungumzo lakini hawajihusishi na utumiaji wa dawa za kulevya. Vilevile mtafiti aliwafanyia usaili askari jamii ambao wanapatika katika eneo analoishi mtafiti. Hivyo, baada ya kupima muongozo wa usaili mtafiti alifanyia marekebisho kasoro alizobaini kabla ya kwenda kuwafanyia usaili watoa taarifa.

3.8.2 Kuaminika kwa data

Best na Khan (2006) wanaeleza kuwa kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kuzalisha matokeo yaleyale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu hizo. Kuaminika kwa data hujitokeza pale ambapo kunakuwa na uhusiano wa taarifa zilizotolewa na watu walewale kwa muda tofauti (Furlong na Lovelace 1999). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikiwa kwa kutumia mbinu tatu za ukusanyaji wa data zilizoainishwa katika sehemu ya mbinu za kukusanyia data (3.5)

3.9 Miiko na maadili ya utafiti

Mtafiti amejitahidi kufuata maadili na miiko yote ya utafiti. Kabla ya utafiti wake aliomba vibali vya ruhusa kutoka taasisi zinazohusika. Vilevile, mtafiti aliomba ridhaa kwa wasailiwa wake na kuwahakikishia kuwa data watakazozitoa ni kwa ajili ya utafiti tu, na sio kwa madhumuni mengine yoyote. Taarifa zote walizotoa zitakuwa ni siri kati ya mtafiti na watoa taarifa.

3.10 Hitimisho

Sura hii imefafanua namna ya utafiti ulivyofanyika. Kipengele cha kwanza ambacho ni mbinu za kukusanyia data alizotumia mtafiti zimeelezwa, mipaka ya utafiti, mbinu za usampulishaji wa watoa taarifa. Pia utaratibu mzima wa ukusanyaji wa data ulivyokuwa na mwisho imeelezea mbinu za kuchambua na kuchanganua data. Katika sura ya nne inayofuata, mtafiti amewasilisha na kuchambua data za utafiti huu.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Utafiti unahusu maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Jumla ya maneno mia moja na sita (106) yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya yalikusanywa. Maneno hayo yalikusanywa katika nyumba za kurekebisha tabia za waathirika wa dawa za kulevya, kliniki za waathirika wa dawa za kulevya, maskani za waathirika wa dawa za kulevya, kutoka kwa wazazi/walezi, walimu na askari wanaopambana na dawa za kulevya. Data za utafiti huu zimepatikana kwa kutumia njia tatu; njia ya mjadala wa kundi lengwa, usaili na ushuhudiaji.

Uchambuzi wa data katika utafiti huu, umezingatia malengo mahsusi ya utafiti. Malengo hayo ni; kubainisha maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar, kuchambua maana zilizofichikana, kueleza sababu za utumiaji wa maana fiche na kutathmini kuhusu athari za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

4.2 Ubainishaji wa maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya

Kwa kuanzia na lengo mahususi la kwanza ambalo ni kubainisha maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la kwanza lililokusudia kutaka kubainisha maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya

Zanzibar. Mtafiti alikusanya maneno mengi kabla ya kuyafanyia upembuzi kutoka katika orodha hiyo ya maneno. Jumla ya maneno mia moja na sita (106) yalionekana kuwa na viashiria vya maana fiche. Maneno hayo ndiyo yaliyofanyiwa kazi ya uchambuzi katika utafiti huu kwa kuongozwa na NmM na NkM.

4.2.1 Maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya

Maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar yamebainishwa katika sehemu hii. Maneno hayo yamekusanywa kwa kutumia mjadala wa kundi lengwa, usaili na ushuhudiaji kwa waathirika 40 wa dawa za kulevya waliopo katika maskani, kliniki na katika nyumba za kurekebishia tabia za waathirika wa dawa za kulevya.

Mtafiti amebaini kuwa, maneno hayo yapo katika makundi makuu matatu ya lugha; maneno yenye asili ya lugha ya Kiswahili, maneno yenye asili ya lugha ya Kigeni (LgzK) na maneno ya kubuni (MyK) yasiyofungamana na lugha yoyote. Ubainishaji wake umeoneshwa katika jadweli na. 4.1 hapa chini.

Jadweli Na. 4.1: Asili ya msamiati

Na	Lugha		Mifano ya Maneno Kutoka Makundi Tajwa	Idadi	Asilimia
1	Kiswahili		<i>Sembe, Mabovu, Mazuri, Bomu, Roho inapenda, Njaa kali na Cheua.</i>	65	61.3
2	MyK		<i>Nambwinya, Ngada, Skanka, Kizidrai, Jojiwea naSadari.</i>	21	19.8
3	LgzK	Kiingereza	<i>Kraki, Brauni, Pusha, Dokta, Faza, Pepa, Waiti, Haba, Blandi, Stiki.</i>	16	15.1
		Kiarabu	<i>Arifu</i>	1	0.9
		Kijerumani	<i>Arosto</i>	1	0.9
		Kifaransa	<i>Rizla</i>	1	0.9
		Kiispania	<i>Gontenamu</i>	1	0.9
Jumla Kuu				106	100

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Kama inavyoonekana katika jadweli hilo, jumla ya waathirika wa dawa za kulevya 40 kati ya 73 (watoa taarifa wote) sawa na asilimia 54.7 wamebainisha maneno yenye maana fiche ambayo hutumia katika mazungumzo baina yao. Data zinaonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi kundi la maneno ya lugha ya Kiswahili. Kundi hilo lilikuwa na maneno sitini na tano (65) kati ya 106 yaliyokusanywa ambayo ni sawa na asilimia 61.3. Kundi la pili lililofuatia ni lile la maneno ya kubuni (MyK) ambalo lilikuwa na jumla ya maneno ishirini na moja (21) kati ya 106 sawa na asilimia 19.8. Kwa upande mwingine

kundi la maneno yenye asili ya lugha za kigeni (LgzK) ndilo lililobainika kuwa na idadi ndogo zaidi ya maneno kwa kuwa na jumla ya maneno ishirini (20) kati ya 106 sawa na asilimia 18.9.

Lengo kuu la NkM ni kuonesha sababu za kubadili mtindo wa kimatamshi na kimsamiati katika kufanya mawasiliano katika jamii inayohusika. Hivyo katika sehemu hii, mtafiti ametumia nadharia hii kuangalia namna watumiaji wa lugha wanavyobadili aina ya maneno kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine ili kufanikisha mawasiliano yao kirahisi. Kwa mantiki hiyo, mtafiti amebainisha maneno yenye maana fiche kwa kuzingatia lugha asili ya maneno hayo sambamba na ubunifu wa maneno yasiyofungamana na lugha yoyote. Wakati wa mjadala, waaathirika wa dawa za kulevya wameeleza kuwa, huyatumia maneno ya kawaida yakiwa na maana tofauti na maana ya msingi ya maneno hayo. Ndani ya makundi ya lugha yaliyobainishwa katika jadweli na. 4.1 kila kundi moja limebainika kuwa na miundo tofauti ya maneno kama inavyoelezwa hapo chini. Inafaa ikumbukwe kwamba, kuna uhusiano baina ya miundo/ maumbo ya maneno na maana ya maneno hayo. Hivyo, ili kufikia mafanikio ya uchambuzi wa maana fiche za maneno ya waathirika wa dawa za kulevya kama ilivyodokezwa katika mipaka ya utafiti (1.6). Sehemu inayofuata imeonesha miundo ya maneno yaliyokusanywa kutoka kwa waathirika wa dawa za kulevya.

4.2.1.1 Miundo ya maneno ya Kiswahili

Mtafiti amefanya uchunguzi wa maneno yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Katika uchunguzi huo, amebaini hali tatu za miundo ya maneno ya Kiswahili yaliyokusanywa. Hali ya kwanza inahusu muundo wa maneno, hali ya pili inahusu aina za maneno na hali ya tatu inahusu matumizi ya virai. Hali hizi tatu zimefafanuliwa kama ifuatavyo.

4.2.1.1.1 Muundo wa maneno

Katika kipengele cha muundo wa maneno yenye asili ya lugha ya Kiswahili yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya, mtafiti amebaini kuwa waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar huunda baadhi ya maneno kwa muambatano wa maneno matatu, muambatano wa maneno mawili na maneno ya kawaida yaliyoundwa kwa neno moja.

4.2.1.1.1.1 Maneno ambatani ya maneno matatu

Katika utafiti huu, yamebainika maneno yaliyoundwa kwa njia ya muambatano wa maneno matatu. Jumla maneno 03 yalikuwa katika muundo huo ambayo ni sawa na asilimia 4.6 ya maneno ya Kiswahili. Mifano ya maneno hayo itaoneshwa katika jadweli namba 4.2.

4.2.1.1.1.2 Maneno ambatani ya maneno mawili

Kwa upande mwingine, mtafiti amebaini pia maneno yaliyoundwa kwa njia ya muambatano wa maneno mawili. Jumla maneno 20 yalikuwa katika muundo huo ambayo ni sawa na asilimia 30.8 ya maneno ya Kiswahili. Mifano ya maneno hayo itaoneshwa katika jadweli namba 4.2.

4.2.1.1.1.3 Neno moja

Katika kipengele hiki mtafiti amebaini kuwepo kwa maneno yaliyoundwa kwa njia mbalimbali lakini yakiwa huru bila kuambatanishwa na neno jingine. Kundi hili lilikuwa na jumla maneno 42 ambayo ni sawa na asilimia 64.6 ya maneno ya Kiswahili. Mifano ya maneno hayo inaoneshwa katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Na. 4.2: Muundo wa maneno

Na	Muundo wa Neno	Mfano wa Msamiati	Jumla	Asilimia
1	Matatu	<i>Sumu ya mawe, mwanamke wa kihindi</i>	03	4.6
2	Mawili	<i>Kudaka sumu, Ngumukumeza.</i>	20	30.8
3	Moja	<i>Bomu, Mwana, Mshindo, Nguo, Chuma,</i>	42	64.6
Jumla Kuu			65	100

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi kundi la tatu la maneno yenye maana fiche. Hili ni kundi la maneno ambalo limeundwa kwa neno moja tu. Kundi hili limebainika kuwa na jumla ya maneno 42 sawa na asilimia 64.6 ya maneno yenye asili ya lugha ya Kiswahili kama inavyoonekana katika jadweli. Kundi la pili ni la maneno ambayo yameundwa kwa muambatano wa maneno mawili. Katika kundi hili, utafiti umebaini jumla ya maneno 20 ambayo ni sawa na asilimia 30.8 ya maneno yote yenye asili ya lugha ya Kiswahili yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Kundi la tatu ni lile lenye maneno yaliyoundwa kwa njia ya

muambatano wa maneno matatu. Kundi hili lilibainika kuwa na maneno 03 Sawa na asilimia 4.6 ya maneno yote ya Kiswahili yaliyochunguzwa.

4.2.1.1.2 Aina za maneno ya Kiswahili

Katika ubainishaji wa maneno yenye asili ya Kiswahili, mtafiti alitaka kujua mchomozo wa aina za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulenya. Katika hali hiyo, aina nne za maneno zilibainika kutumiwa na waathirika hao. Kati ya maneno 65 ya Kiswahili, maneno 8 yalikuwa vitenzi sawa na asilimia 19. Maneno 23 yalikuwa Nomino sawa na asilimia 54.8. Maneno 4 yalikuwa vivumishi ambayo ni sawa na asilimia 9.5. Mwisho ni vielezi ambavyo vilikuwa 7 sawa na asilimia 16.6 ya maneno yote ya Kiswahili. Jadweli lifuatalo linabainisha kwa uwazi idadi na asilimia ya aina hizo za maneno.

Jadweli Na. 4.3: Aina za maneno ya Kiswahili

Na	Aina za Maneno	Mifano ya msamiati	Idadi	Asilimia
1	Nomino	<i>Maji, nyuki, karanga.</i>	23	54.76
2	Vitenzi	<i>Tapika, cheua, kudaka.</i>	8	19.04
3	Vivumishi	<i>Mabovu, mazuri, mkali.</i>	4	9.52
4	Vielezi	<i>Kitunduni, mihemo, waki hindi</i>	7	16.66
Jumla Kuu			42	100

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Uchambuzi wa aina za maneno ya Kiswahili yaliyokusanywa katika utafiti huu, imebainika kuwa waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi nomino kuliko aina nyingine za maneno. Kwa upande mwingine imebainika matumizi madogo ya vivumishi na hakukuwa na aina nyingine za maneno uliobainika.

4.2.1.1.3 Matumizi ya virai

Imebainika pia matumizi ya virai katika data zilizokusanywa. Sio wakati wote waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno pekee. Kuna wakati huunganisha maneno na kufanya virai vinavyobeba maana fiche mbalimbali kulingana na muhtadha wao. Katika data zilizokusanywa jumla ya virai 23 vilibainika ambavyo ni sawa na asilimia 35.4. Virai hivyo vimejengwa kwa kategoria mbalimbali za maneno kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Na. 4.4: Matumizi ya virai

	Kirai	Muundo wa Kirai
1	<i>Roho inapenda,</i>	$N + T$
2	<i>Njaa kali</i>	$N + V$
3	<i>Kudaka sumu</i>	$T + N$
4	<i>Supu ya mawe</i>	$N+H+N$
5	<i>Mwanamke wa kihindi</i>	$N+H+E$
6	<i>Mzee wa utamu</i>	$N + H + E$

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Data za utafiti huu zimeonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi virai vilivyoundwa kwa maneno mawili kuliko vile vilivyoundwa kwa maneno matatu. Virai vya aina ya kwanza vilikuwa 13 sawa na asilimia 56.5 na virai vya aina ya pili vilikuwa kumi (10) sawa na asilimia 43.5.

Ingawa matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi maneno ambayo yameundwa kwa neno moja yenye maana fiche kuliko maneno

yalioambatanishwa na kuwa virai. Aina hiyo ya maneno ilikuwa na maneno 42 sawa na asilimia 64.6 ya maneno yote yenye asili ya lugha ya Kiswahili.

4.2.1.2 Miundo ya maneno ya kubuni

Kwa upande wa MyK utafiti umebaini kwamba, waathirika wa dawa za kulevya hubuni maneno mapya ili kukidhi haja ya mawasiliano. Data zinaonesha kuwa yapo MyK ambayo yameundwa kwa silabi moja, silabi mbili, silabi tatu na silabi nne. Vilevile imebainika kuwa silabi zilizomo katika MyK zimeundwa kwa kufuata utaratibu wa miundo ya silabi za Kiswahili. Idadi za silabi katika maneno hayo zimechambuliwa kwa kina. Hivyo mtafiti amechambua miundo ya MyK kwa kutazama vipengele vitatu; idadi ya silabi zilizounda neno, aina za silabi zilizounda neno na miundo ya silabi zilizomo katika MyK yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

4.2.1.2.1 Idadi ya silabi zilizounda maneno ya kubuni

Katika ubainishaji wa idadi ya silabi katika MyK, mtafiti amechunguza idadi ya sauti ambazo hutamkwa mara moja, kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Data zinaonesha kuwa, MyK huundwa kwa silabi mbili, tatu au nne. Jadweli lifuatalo linabainisha MyK na idadi ya silabi.

Jadweli Na. 4.5: Idadi ya Silabi Katika Maneno ya Kubuni

Na.	Mfano	Silabi	Uchambuzi	Idadi ya maneno	Asilimia
1	<i>Widi</i>	2	Wi+di	3	14.3
2	<i>Nambwinya</i>	3	<i>Na + mbwi + nya</i>	11	52.4
3	<i>Vyakudanki</i>	4	<i>Vya+ku+da+nki</i>	7	33
	Jumla			21	100

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Mtafiti amebaini kuwa, idadi kubwa ya MyK yameundwa kwa silabi tatu. Data zimeonesha jumla ya MyK kumi na moja (11) sawa na asilimia 52.4 yameundwa kwa silabi tatu. Kundi linalofuatia kwa wingi wa MyK ni lile lenye silabi nne ndani yake. Katika kundi hili, Jumla ya maneno saba (7) sawa na asilimia 33 yamebainika kuundwa kwa silabi nne. Aidha, kundi la MyK yenye silabi mbili limebainika kuwa na idadi ndogo ambalo lina maneno matatu (3) sawa na asilimia 14.3. Kwa ujumla, waathirika wa dawa za kulevywa hubuni zaidi maneno yenye silabi tatu.

4.2.1.2.2 Aina za silabi zilizounda maneno ya kubuni

Data zinaonesha kuwa, MyK yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevywa yanazingatia aina za silabi za lugha ya Kiswahili. Katika lugha ya Kiswahili kuna aina kuu mbili za silabi. Aina hizo ni silabi huru na silabi funge. Silabi huru ni aina ya silabi ambayo huishia na irabu na silabi funge ni aina ya silabi ambayo huishia na

konsonanti. Aina hizo ndio ambazo zimebainika katika MyK yenye maana fiche unaotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar kama zinavyoonyeshwa katika jadweli lifuatalo.

Jadweli Na. 4.6: Aina za silabi katika maneno ya kubuni

Na.	Mfano wa maneno	Aina za silabi	Uchambuzi	Silabi huru/silabi funge	Idadi ya maneno	Asilimia
1	<i>Sadari</i>	Huru	<i>Sa + da + ri</i>	'Sa' 'da' 'ri'	15	71.4
2	<i>Mchokocho</i>	Funge	<i>M+cho+ko+cho</i>	'M'	6	28.6
Jumla					21	100

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, kundi la kwanza la aina za silabi (silabi huru) lina idadi kubwa ya MyK yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Jumla ya MyK 15 sawa na asilimia 71.4 yameundwa kwa silabi huru. Kwa upande wa silabi funge, utafiti umebaini maneno sita 6 ya kubuni ambayo ni sawa na asilimia 28.6 yameundwa kwa mchanganyiko wa silabi huru na silabi funge. Katika jadweli

na 4.6, aina za silabi zimebainishwa kwa wino uliokolezwa katika mifano ya MyK yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

4.2.1.2.3 Muundo wa silabi katika maneno ya kubuni

Katika lugha ya Kiswahili maneno huundwa kwa kufuata miundo maalumu ya silabi.

Miundo hiyo ni ya aina kuu tano;

- Muundo wa konsonanti pekee (K).
- Muundo wa irabu moja pekee (I).
- Muundo wa konsonanti moja na irabu moja (KI).
- Muundo wa konsonanti mbili zilizofatana na kumalizikia na irabu moja (KKI); na
- Muundo wa konsonanti tatu zilizofatana na kumalizikia na irabu (KKKI).

Miundo hii pia imebainika katika MyK yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya kama inavyochambuliwa katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Na. 4.7: Muundo wa silabi Katika maneno ya kubuni

Na.	Mfano wa Neno	Silabi	Muundo wa silabi	Idadi	Asilimia
1	<i>M+dananda</i>	<i>M</i>	K	6	28.6
2	<i>shwa + i + ni</i>	<i>I</i>	I	4	19
3	<i>mu +ki + de</i>	<i>'Mu' 'ki' 'de'</i>	KI	7	33
4	<i>Vya+ku+da+nki</i>	<i>'Vya' 'nki'</i>	KKI	3	14.3
5	<i>Na+mbwi +nya,</i>	<i>Mbwi</i>	KKKI	1	4.8
JUMLA				21	100

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Jadweli hili linaonesha kuwa, maneno yanayobuniwa na waathirika wa dawa za kulevya hufuata miundo ya silabi za lugha ya Kiswahili. Idadi kubwa ya MyK huundwa kwa kutumia muundo wa konsonanti na irabu. Jumla ya maneno saba (7) ya kubuni sawa na asilimia 33 yameundwa kwa kufuata muundo huo. Muundo wa pili wa silabi uliobainika kutumika kubuni maneno ni muundo wa konsonanti pekee. Muundo huo umebainika katika maneno sita (6) ya kubuni sawa na asilimia 28.6. Muundo mwingine wa silabi katika MyK ni muundo wa irabu pekee. Muundo huu umebainika katika maneno manne (4) sawa na asilimia 19. Vilevile muundo wa konsonanti mbili na irabu moja umebainika kutumika katika baadhi ya maneno. Jumla ya maneno matatu (3) ya kubuni sawa na asilimia 14.3 yameundwa kwa muundo huo wa silabi. Sambamba na hayo, utafiti pia umebaini muundo wa silabi wa konsonanti tatu na irabu. Muundo huu hutumiwa kwa kiasi kidogo sana katika kubuni maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Neno moja limebainika kuundwa kwa kutumia muundo huo ambalo ni sawa na asilimia 4.7.

4.2.1.3 Maneno yenye asili ya lugha za kigeni

Data zinaonesha kuwa, katika kundi la maneno yenye asili ya LgzK, Kiingereza kimeonekana kutumika zaidi kuliko lugha nyingine. Kwa ujumla utafiti umebaini lugha tano za kigeni (Kiingereza, Kiarabu, Kifaransa, Kijerumani na Kihispania) zilizotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya zina jumla ya maneno 20 kati ya 106 ambayo ni sawa na asilimia 18.9. Watoa taarifa wameeleza kwamba, mara nyingi wanapotamka maneno yenye asili ya lugha za kigeni huyatamka kwa kufuata kanuni za matamshi ya lugha ya Kiswahili.

4.2.1.3.1 Ubainishaji wa matamshi ya maneno

Kwa kuanzia na matamshi ya maneno yenye asili ya lugha za Kigeni, utafiti umebaini waathirika wa dawa za kulevya hutamka maneno kwa kuvuta irabu za mwisho za maneno hayo. Uvutaji huo wa sauti umebainika kwa waathirika wa dawa za kulevya tu. Hali hii huwachanganya watumiaji wengine wa lugha wasiotumia dawa za kulevya. Baadhi ya wakati hushindwa kuelewa maana ya maneno na hata kushindwa kuyatambua maneno yanayohusika kutokana na namna maneno hayo yalivyotamkwa. Jadweli lifuatalo linabainisha tofauti ya matamshi ya maneno katika LgzK na matamshi ya waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Jadweli Na. 4.8: Matamshi ya Maneno

Na.	Asili ya Maneno	Mfano wa Neno	Matamshi Asili	Matamshi ya Waathirika
1	Kiarabu	<i>Arifu</i>	/عارف/	/arifu:/
2	Kijerumani	<i>Arosto</i>	/ar'rosto/	/arosto:/
3	Kifaransa	<i>Rizla</i>	/rizlə/	/rizla:/
4	Kihispania	<i>Gontenamu</i>	/gwæn,tænəməʊ/	/gɔŋtenamu:/
5	Kiingereza	<i>Blandi</i>	/bland/	/blandr:/

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Mtafiti ameshuhudia waathirika wa dawa za kulevya wakitamka maneno yenye asili ya lugha za kigeni. Alibaini hufuata sheria za matamshi ya lugha ya Kiswahili kama vile uambishaji wa irabu mwishoni mwa maneno yanayoishia na konsonanti. Mfano katika

neni *bland* irabu /i/ imeambishwa, hatimaye neno hilo likabadilika kutoka /bland/ kuwa /blandɪ/. Lugha ya Kiswahili huambisha irabu moja lakini waathirika wa dawa za kulevya wao huambisha irabu mbili zenye sifa sawa. Mfano /blandɪ/ na kuwa /blandɪ:/. Hali hii ya uambishaji wa irabu mbili si kwa maneno yanayoishia na konsonanti tu bali pia kwa maneno yanayoishia na irabu. Mfano /rɪzlə/ hubadilika na kuwa /rizla:/.

4.2.1.3.2 Aina za maneno yenye asili ya lugha za kigeni

Data zinaonesha aina tatu za maneno yenye asili ya lugha za kigeni yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Aina hizo ni nomino, vivumishi na vitenzi. Jadweli lifuatalo linabainisha idadi na asilimia za aina hizo za maneno:

Jadweli Na. 4.9: Aina za Maneno ya Lugha za Kigeni

Na	Aina	Mfano wa Maneno	Jumla	Asilimia
1	N	<i>Gontenamu, Faza, rizla, Arifu, Stiki.</i>	8	50
2	V	<i>Arosto, Blandi, drai, kalm, brevu</i>	5	31.2
3	T	<i>Shuti, swipi, draivu,</i>	3	18.8
Jumla			16	100

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Kutokana na takwimu za jadweli la hapo juu, idadi kubwa ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya yanayotoka katika LgzK ni nomino. Jumla ya nomino (8) sawa na asilimia 40 zimebainika. Vivumishi pia vimebainika katika utafiti huu. jumla ya maneno matano (5) sawa na asilimia 25 yalikuwa katika kundi la vivumishi. Kwa upande

mwingine idadi ndogo ya vitenzi ilibainika. Vitenzi vilikuwa 3 sawa na asilimia 15 ya maneno yote yenye asili ya LgzK.

4.3 Ufafanuzi wa maana fiche za msamiati

Lengo la pili la utafiti huu ni kufafanua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la pili lililouliza: Ni zipi maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar? Imebainika kwamba, waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno ya kawaida ambayo maana yake ya msingi huwa inafahamika kwa wanajamii wote. Hata hivyo wao (waathirika wa dawa za kulevya) huyabebesha maneno hayo maana mpya (fiche). Sambamba na hayo, waathirika wa dawa za kulevya hubuni maneno mapya ambayo hayajulikani na wanajamii na kuyatumia kwa lengo la kukidhi mawasiliano baina yao. Si hayo tu, waathirika wa dawa za kulevya pia hutumia maneno ya LgzK kama ilivyoelezwa katika sehemu iliyotangulia.

Nadharia ya Maana ni Matumizi ndiyo inayouongoza ufafanuzi wa maana fiche za maneno kama ilivyodokezwa hapo kabla. Mhimili wa Nadharia ya Maana ni Matumizi inayohusika katika uchambuzi wa maana fiche za maneno haya ni ule unaoeleza kwamba maana ya maneno hufasiliwa kwa mujibu wa watumiaji wake. Kwa hivyo katika kipengele hiki waathirika wa dawa za kulevya ambao ndio watumiaji wa maneno hayo ndio waamuzi wa maana fiche za maneno hayo.

Utafiti umebaini kwamba, waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar hutumia maana fiche wanapobainisha aina za dawa za kulevya, vipimo vya dawa za kulevya, vifungashio vya

dawa za kulevya, maana fiche zinazohusu taasisi zinazopambana na dawa za kulevya, maneno yanayobainisha majina ya wauzaji wa dawa za kulevya pamoja na maneno yanayotumika kuwadhihaki vijana wasiotumia dawa za kulevya. Hivyo, data zimefafanuliwa kwa mujibu wa makundi matano yaliyotajwa hapo juu.

4.3.1. Aina za dawa za kulevya

Kutokana na uchambuzi wa data imebainika kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia maana fiche wanapobainisha aina za dawa za kulevya wanazotumia. Waathirika wote 40 wa dawa za kulevya wamethibitisha uwepo wa matumizi ya aina sita za dawa za kulevya katika Mkoa wa Mjini Magharibi na kwamba huzipa majina yenye maana fiche. Dawa hizo za kulevya ni; Pombe, Unga, Bangi, Vidonge, Mirungi na Charas. Jadwali na. 4.10 linaonesha aina za dawa za kulevya na majina yake.

Jadweli Na. 4.10: Maana Fiche katika Majina ya Dawa za Kulevya

Na.	Aina	Majina Yanayotumika	Jumla	Asilimia
1	Bangi	<i>Rizla, Mchokocho, Majani, Haba, Blandi, Kwida, Kaya, Chicha, Mtorijo, Widi, Stiki, Aguli, Msuba, Dongo</i>	14	36.8
2	Pombe	<i>Chuma, Ngumu kumeza, Kosovo, Kachaso, Supu ya mawe</i>	05	13.6
3	Vidonge	<i>Njugu, Karanga, Vyakudanki, Nomemori, Shwaini, Kwarukwaru, Njunja</i>	07	18.4
4	Unga	<i>Sumu, Dawa, Roho inapenda, Brauni, Pele, Kraki, Kichupa, Musharafu</i>	08	21
5	Mirungi	<i>Tembele, Chakusaga</i>	02	5.2
6	Charas	<i>Hashi, Gundi</i>	02	5.2
Jumla Kuu			38	100

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020).

Matokeo ya utafiti yamebaini kwamba, dawa moja ya kulevya imepewa majina zaidi ya moja yenye maana fiche. Hii ni kwa sababu ya kumrahisishia muuzaji wa dawa za kulevya kumtambua mteja wake na eneo analotokea. Hivyo, muuzaji wa dawa za kulevya anapozungumza na mteja wake huweza kumtambua kirahisi mahali anapotokea. Mkakati

huu hulenga kulinda usalama wake muuzaji, endapo atakwenda mteja ambaye atatumia maneno yasioeleweka hutilia mashaka. Hapo humlazimu muuzaji kuwa makini na kufanya uchunguzi juu ya uhalali wa mteja huyo ndipo apate huduma. Sababu nyingine inayosababisha dawa moja ya kulevya kuwa na majina mengi ni kuzoeleka kwa jina moja na kutambulika maana yake kwa wanajamii. Hivyo watumiaji wa dawa za kulevya hulazimika kuunda jina (neni) jipya wanapohisi kuwa wanajamii tayari wameshafichua maana ya jina linalotumika kwa wakati huo. Hapo jina la awali huanza kufinyaa na baadae kufa au hutumika mara chache kwa umakini mkubwa. Kwa mfano, tunaona katika jadweli na. 4.10 hapo juu, bangi imekuwa na majina kumi na nne (14) kati ya 38 sawa na asilimia 36.8, Vidonge vina majina saba (7) sawa na asilimia 13.6, Unga una majina nane (8) sawa na asilimia 18.4, Pombe nayo ina majina matano (5) sawa na asilimia 21, Mirungi na Charas kila moja ina majina mawili (2) ambayo ni sawa na asilimia 5.2.

Jumla ya watoa taarifa 13 kati ya 40 sawa na asilimia 32.5 ya waathirika wote walifanyiwa usaili. Usaili huo ulifanyika kutoka katika nyumba za kurekebisha tabia na kliniki za waathirika wa dawa za kulevya. Katika usaili walieleza kuwa, dawa za kulevya zenye majina mengi ya uficho ni dawa ambazo hupigwa vita zaidi hapa Zanzibar na hutumiwa kwa siri zaidi kuliko zenye majina machache. Hapa ndipo Nadharia ya Maana ni Matumizi inavyoakisi uhalisia wake. Mhimili wa Nadharia ya Maana ni Matumizi unasisitiza umuhimu wa kuwashirikisha watumiaji (wazungumzaji) wa lugha ili kupata maana ya neno. Katika utafiti huu imebainika kuwa waathirika wa dawa za kulevya hutumia majina

yenye maana fiche ambayo wanayatambua wao tu. Hivyo bila ya kuwahusisha wenyewe ingekuwa vigumu kupata maana halisi fiche iliyokusudiwa.

4.3.2. Vipimo vya dawa za kulevya

Waathirika wa dawa za kulevya hutumia maana fiche katika majina ya vipimo vinavyotumika kupima dawa za kulevya. Jumla ya waathirika 25 wamefanya mjadala na mtafiti katika nyumba za kurekebisha tabia pamoja na wale wanaohudhuria kliniki ya waathirika wa dawa za kulevya. Katika mjadala huo, wameeleza kwamba, dawa za kulevya huuzwa kwa siri sana. Wauzaji na watumiaji hutumia maneno yenye maana fiche katika vipimo vyao ili wasitambulike na wanajamii au kutuhumiwa na vyombo vya usalama. Ili kupata maana ya maneno yanayotumiwa katika vipimo vya dawa za kulevya, Nadharia ya Maana ni Matumizi ndio iliyomuongoza mtafiti kuyachunguza maneno hayo na kupata ufafanuzi wake kutoka kwa watumiaji wenyewe wa dawa za kulevya ambao ndio watumiaji wa maneno hayo. Nadharia ya Maana ni Matumizi inasisitiza kuwahusisha watumiaji wa lugha ili kupata maana ya kile kilichozungumzwa. Jadweli na. 4.11 linaonesha vipimo vya dawa za kulevya na maana zake kwa mujibu wa watoa taarifa.

Jadweli Na. 4.11 Majina ya vipimo vya dawa za kulevya

Na	Aina ya Dawa	Kipimo	Maana
1.	Bangi	<i>Nyongo</i>	Bangi iliyosokotwa kama sigara
2	Unga	<i>Kete</i>	Unga uliofungwa katika karatasi maalumu
3	Pombe	<i>Jojiwea,</i>	Lita moja na nusu ya pombe
		<i>Jibuti</i>	Glasi moja ya pombe
		<i>Nusu</i>	Pombe nusu gilasi
		<i>Nibu</i>	Pombe robo gilasi
4	Vidonge	<i>Busta</i>	Kidonge kimoja
5	Mirungi	<i>Kicha</i>	Fungu la mirungi

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020).

Watoa taarifa wameeleza kwamba, kipimo cha bangi huitwa *nyongo*. Nyongo ni bangi iliyosokotwa katika mfumo wa sigara. Hivyo, mtumiaji wa bangi huweza kutumia nyongo kulingana na mahitaji yake. Mfano; wapo ambao hutumia nyongo moja (bangi moja), mbili na kuendelea. Kwa upande wa unga kipimo chake huitwa *kete*. Kete ni kipimo cha kwanza cha unga uliofungwa katika karatasi maalumu. Waathirika wa dawa za kulevya huweza kutumia kete moja au zaidi kulingana na uwezo wake wa kifedha na kimatumizi. Pombe nayo ina vipimo vya aina nne ambavyo ni *Jojiwea, Jibuti, Nusu, Nibu*. *Jojiwea* hiki ni

kipimo cha lita moja na nusu ya pombe, *Jibuti* ni kipimo cha gilasi iliyojaa pombe, *Nusu* ni nusu gilasi ya pombe, *Nibu* ni robo glasi ya pombe kama ilivyoielezwa hapo kabla.

Vilevile vidonge vya dawa za kulevya huuzwa na kutumiwa kulingana na mahitaji ya mtumiaji. Kidonge kimoja huitwa *busta*, viwili huitwa busta mbili na kuendelea. *Kicha* ni fungu moja la mirungi, mafungu mawili huitwa kicha mbili na kuendelea. Hivyo, maana fiche za vipimo vya dawa za kulevya zimepatikana kwa mujibu wa watumiaji katika muktadha unaohusika kama ambavyo Nadharia ya Maana ni Matumizi inavyoelekeza.

4.3.3. Vifungashio vya dawa za kulevya

Katika utafiti huu, mtafiti amefanikiwa kubaini majina ya vifungashio mbalimbali vya dawa za kulevya. Katika maskani za waathirika wa dawa za kulevya, mtafiti amewasikia waathirika wa dawa za kulevya wakitaja maneno; *sanda, nguo, pepa na waiti*. Kwa kuwa lengo la pili la utafiti huu limeongozwa na Nadharia ya Maana ni Matumiazi ambayo inahimiza uhusishwaji wa watumiaji wa lugha katika upatikanaji wa maana ya neno, mtafiti baada ya kuwashuhudia waathirika wa dawa za kulevya waliopo maskanini hapo alifanya mjadala na waathirika 5 kati ya 10 ambao ni sawa na asilimia 50 ya waathirika wanaohudhuria kliniki ya waathirika wa dawa za kulevya (Mati kliniki) iliyopo Kidongo Chekundu. Katika mjadala huo, maana fiche za majina yanayotumika kama vifungashio zilibainika. Utafiti umebaini kuwepo kwa majina manne yanayorejelea karatasi inayotumiwa kusokotea bangi ili kuifanya iwe mfano wa sigara na iweze kuvutika. Jadweli

na. 4.12 linaonesha majina hayo ya vifungashio vya bangi pamoja na maana zake (maana ya msingi na maana fiche).

Jadweli Na. 4.12: Majina ya Vifungashio vya Bangi

Na.	Vifaa	Maana ya msingi	Maana fiche
1	<i>Sanda</i>	Kitambaa cheupe anachovikwa maiti wa Kiislamu kwa utaratibu maalumu na kuzikwa nacho	Karatasi ya kusokotea bangi kwa ajili ya kuvuta
2	<i>Nguo</i>	Vazi au kitambaa chochote	Karatasi ya kusokotea bangi
3	<i>Pepa</i>	Karatasi	Karatasi ya kusokotea bangi
4	<i>Waiti</i>	Nyeupe	Karatasi ya kusokotea bangi

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020).

Data zinaonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno ya kawaida katika kubainisha vifungashio vinavyotumika kufungia au kusokotea dawa ya kulevya kwa ajili ya matumizi. Maneno wanayotumia ni yale yanayoeleweka na wanajamii. Ingawa hivyo, wao huyatumia kwa maana tofauti na ile ya msingi. Vifungashio hivyo hutumika kusokotea bangi kama ilivyoelezwa. Maneno *sanda* na *nguo* ni maneno sanifu ya lugha ya

Kiswahili yanayoeleweka na wanajamii wote. Kwa watumiaji wa bangi maneno hayo, huwa na maana nyingine fiche wanayoielewa wao tu. Vilevile maneno *waiti* na *pepa* ni maneno sanifu ya lugha ya Kiingereza na hutumiwa na wanajamii kwa maana ileile ya msingi kutoka lugha ya Kiingereza. Kwa waathirika wa dawa za kulevyo, maneno haya huwa na maana fiche kama ilivyoonyeshwa katika jadweli na. 4.12.

4.3.4. Taasisi zinazopambana na dawa za kulevyo

Utafiti umebaini kuwa, waathirika wa dawa za kulevyo hutumia maana fiche wanapopeana taarifa kuhusiana na taasisi zinazopambana na dawa za kulevyo. Hali hii hukwamisha mapambano dhidi ya dawa za kulevyo nchini. Lengo la kutokomeza dawa za kulevyo nchini hushindwa kufikiwa. Ifuatayo ni mifano mbalimbali ya maneno yenye maana fiche inayobainisha taasisi zinazopambana na dawa za kulevyo.

Jadwali Na. 4.13: Maneno yanayohusu taasisi zinazopambana na dawa za kulevyo

Na.	Taasisi	Maneno Yanayotumiwa
1	Askari	<i>Wadudu, Wazee, Wachawi, Njaakali</i>
2	Kituo cha polisi	<i>Geto</i>
3	Rumande	<i>Kitunduni</i>
4	Gari la polisi	<i>Farasi, Mpira</i>
5	Mpelelezi	<i>Doriani</i>

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Ifuatayo ni mifano ya mazungumzo iliyotolewa na waathirika 4 kati ya 5 sawa na asilimia 80 ya waathirika wa dawa za kulevya. Waathirika hawa wametafitiwa kwa kutumia njia ya mjadala wa kundi lengwa katika nyumba ya kurekebishia tabia iliyopo Bububu. Walimpa mtafiti mifano ya namna wanavyowasiliana kwa kutumia maneno hayo:

- i. *Mazee dorianiiii*
- ii. *Aiii wadudu wamezagaaa.*
- iii. *Nimeuona mpira / farasi wa wazee pale road.*
- iv. *Chafu yangu mpaka sasa yupo geto.*

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Katika mfano wa kwanza neno *doriani* ni neno lenye maana fiche. Maana ya kawaida ni tunda kubwa lenye ncha mithili ya miba nje ya ganda, kokwa kubwa zenye nyama laini na harufu kali (BAKIZA, 2010). Maana fiche ya neno *doriani* kwa waathirika wa dawa za kulevya ni mpelelezi au askari wa upelelezi. Watoa taarifa wengine waliohojiwa wameeleza kuwa, waathirika wa dawa za kulevya wanaposikia neno hilo hushituka na kuanza kuangalia huku na kule. Wakiona hali isiyoieleweka huanza kuondoka mmoja mmoja.

Mfano wa pili, neno *wadudu* ni neno lenye maana fiche linalotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Maana ya kawaida ya neno wadudu ni kiumbe hai chenye gimba lililogawanyika sehemu tatu bayana: kichwa, kifua na fumbatio (BAKIZA, 2010). Waathirika wa dawa za kulevya hutumia neno *wadudu* wakimaanisha askari.

Katika mfano wa tatu, maneno *mpira au farasi* ni maneno ya kawaida yenye maana inayojulikana na wanajamii wote; *mpira* maana yake ni kitu mviringo kilichotengenezwa kwa mpira kwa ajili ya michezo. *Farasi* ni mnyama mkubwa wa kufuga anayefanana na punda mwenye manyoa shingoni na mkia wa singa (BAKIZA, 2010)). Waathirika wa dawa za kulevya huyatumia maneno hayo kwa maana fiche; gari la polisi.

Nalo neno *geto* ni neno ambalo sio rasmi, ambalo kwa kawaida hutumiwa zaidi na vijana wa mitaani, likimaanisha sehemu wanayoishi vijana ambao hawajaoa. Kwa upande wa waathirika wa dawa za kulevya, neno hili limebainika kuwa na maana tofauti kabisa. Wao hutumia neno hilo wakimaanisha kituo cha polisi.

Kwa ujumla, waathirika wa dawa za kulevya wanatambua kuwa utumiaji wa dawa za kulevya ni kinyume cha sheria na wanatambuwa kuwepo kwa taasisi na vyombo mbalimbali vinavyopambana na dawa za kulevya. Hii ndio sababu inayowafanya watumie maana fiche wanapozungumzia kuhusu vyombo na taasisi hizo. Hivyo, watumiaji wa lugha wana nafasi kubwa katika upatikanaji wa maana ya maneno. Ni vigumu sana kubaini maana ya maneno pasi na kumuhusisha mtumiaji au watumiaji kama Nadharia ya Maana ni Matumizi inavyoeleza.

4.3.5. Wauzaji wa dawa za kulevya

Data za utafiti zinaonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno yenye maana fiche kubainisha majina ya wauzaji wa dawa za kulevya. Majina yenye maana fiche

hayo huwatofautisha wasambazaji kutokana na aina za dawa za kulevya wanazouza au kusambaza kama yalivyooneshwa hapo chini katika jadweli na. 4.14

Jadweli Na. 4.14: Majina ya Wauzaji wa Dawa za Kulevya

Na.	Maneno	Maana Fiche
1	<i>Mama supu, mama Kosovo</i>	Muuzza pombe.
2	<i>Pusha, Dokta, Mzungu, Mzee wa utamu, Mkali wao</i>	Muuzaji wa unga, vidonge na Charas.
3	<i>Faza, sadari, taita</i>	Muuzza bangi au mirungi.

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Ifuatayo ni mifano ya matumizi ya maneno yenye maana fiche katika sentensi. Sentensi hizi zimepatikana katika mjadala wa kundi lengwa kwa waathirika wa dawa za kulevya. Mjadala huu ulifayika katika nyumba ya kurekebisha tabia iliyopo Kisauni. Jumla ya watoa taarifa 5 walifanya mjadala na wawili kati yao walitoa mfano wa mazungumzo ya waathirika wa dawa za kulevya kama inavyooneshwa hapo chini.

Mwathirika na. 1: *Leo niko mabovu inabidi tu nikamuone mama supu maana mzee wa utamu sina chakumshikisha*

Mwathirika na. 2: *Twende zetu kwa mkali wao bwana ntakugongea damu yangu.*

Mwathirika na. 1: *Subiri nimpigie mzungu, niko arosto kichizi.*

Mwathirika na. 2: *Mimi acha nimtafute sadari tupate sanda.*

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Mifano ya sentensi hizo inaonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya kwa kiasi kikubwa hutumia maneno ya lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, mtu ambaye si muathirika wa dawa za kulevya hawezi kuelewa kinachozungumzwa. Hii ni kwa sababu ya utumiaji wa maneno yenye maana fiche. Kwa mfano, Mwathirika Na. 1 alikuwa na maana kuwa; *'leo hana pesa ya kutosha inabidi aende kwa muuza pombe kwa sababu muuza unga, vidonge au charas hana cha kumlipa'*. Mwathirika na. 2 anamjibu kuwa *'twende kwa muuza unga rafiki yangu'*. Mwathirika na. 1 anamwambia muathirika na. 2 kuwa, *anampigia simu muuza unga/ vidonge/ charas kwa sababu anapata maumivu kutokana na kukosa dawa za kulevya.* Naye Mwathirika na. 1 anasema kuwa, *anamtafuta muuza bangi anunue karatasi ya kusokotea bangi ili waweze kusokota unga na kuuvuta kwa kutumia pua.*

Kwa ujumla mtafiti amechambua na kufafanua maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Amefanya hivyo kwa muongozo wa Nadharia ya Maana ni Matumizi kama ambavyo lengo kuu la pili la utafiti huu lilivyoelekeza. Mifano ya maneno yenye maana fiche pamoja na ufafanuzi wa maana fiche hizo zote ni kwa mujibu wa watoa taarifa ambao ni waathirika wa dawa za kulevya kutoka katika maskani za wathirika wa dawa za kulevya, kliniki za waathirika wa dawa za kulevya na waathirika ambao wanaishi katika nyumba za kurekebisha tabia. Hivyo, maana haipatikani kwa

kuangalia neno pekee bali hupatikana kwa kuangalia namna gani watu au jamii wanavyolitumia neno hilo katika miktadha tofauti kama Nadharia ya Maana ni Matumizi inavyoelekeza.

4.3.6 Kuwadhihaki vijana wasiotumia dawa za kulevya

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, yapo majina maalumu ambayo hutumiwa na waathirika wa dawa za kulevya kwa ajili ya kuwadhihaki vijana wasiotumia dawa hizo. Hali hii ya kuwadhihaki wasiotumia huwafanya baadhi ya vijana kujiingiza katika kundi hilo ili kujiepusha na kudhihakiwa. Mfano wa majina hayo yameorodheshwa katika jadweli 4.15.

Jadweli Na. 4.15: Majina Yanayotumika Kuwadhihaki Wasiotumia Dawa za Kulevya

Majina	Maana ya Msingi	Maana Fiche
<i>Mwari</i>	Msichana ambaye amebaleghe lakini hajaolewa.	Mtu asievuta bangi
<i>Boga</i>	Tunda kubwa lenye umbo la mviringo, maganda magumu, nyama rangi ya manjano na kokwa nyingi, la mmea jamii ya mtango, linaloliwa baada ya kupikwa.	Mtu asietumia unga
<i>Mdananda</i>	Neno la kubuni.	Mtu asiyetumia dawa yoyote ya kulevya likimfananisha na mwanaume shoga
<i>Kumbi</i>	Ganda la nje la nazi au dafu.	Mtu asiekunywa pombe

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (2020)

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, matumizi ya maneno yenye maana fiche huweza kumfanya mtu kushawishika na kuingia katika utumiaji wa dawa za kulevya. NkM inaeleza kwamba, sababu kuu za kubadili mtindo wa kimatamshi ni kuashiria uhusiano na mafungamano ya watu. Watoa taarifa sita wamethibitisha kuwa, miongoni mwa mambo yaliyowapelekea kushawishika kujiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya ni majina mabaya waliyokuwa wakiitwa na vijana wenzao ambao ni watumiaji wa dawa za kulevya. Hivyo, ili kulinda hadhi na heshima yao wakaona ni vyema kujiunga na kundi hilo.

4.4 Sababu za matumizi ya maana fiche

Lengo la tatu la utafiti huu ni kujadili sababu za matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali lililouliza; ni zipi sababu za matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar? Watoa taarifa wameweza kueleza sababu mbalimbali za utumiaji wa maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Uchambuzi wa sababu za matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar umeongozwa na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na:

4.4.1 Sababu za kiusalama

Baadhi ya watoa taarifa walieleza kwamba, waathirika wa dawa za kulevya hulazimika kutumia maana fiche kwa sababu za kiusalama. Sababu hii imeelezwa kwa kutumia mbinu ya usaili na mbinu ya mjadala wa kundi lengwa. Kwa vile dhamira kuu ya NkM ni kuonesha sababu za kubadili mtindo wa matamshi au maneno ndani ya mawasiliano ya jamii fulani mtafiti amewasaili watoa taarifa pamoja na kufanya nao mijadala. Amefanya hivyo ili kubaini ni sababu zipi haswa zinazosababisha waathirika wa dawa za kulevya watumie maana fiche katika mazungumzo baina yao. Imeelezwa kuwa, waathirika wa dawa za kulevya wanafahamu kuwa utumiaji wa dawa za kulevya ni kunyume cha sheria hivyo, hulazimika kuficha maana ili kujilinda wao wenyewe na kuwalinda wauzaji au wasambazaji. Hufanya hivyo wakiwa na lengo la kujiepusha kukamatwa au kutuhumiwa kutokana na utumiaji, usambazaji na uuzaji wa dawa za kulevya. Sababu hii imeelezwa na

watoa taarifa wote isipokuwa waathirika wa maskani tu. Hivyo watoa taarifa 68 sawa na asilimia 93 wameeleza sababu hii.

4.4.2 Kuweka siri

Sababu nyingine iliyobainika katika uchambuzi wa data za utafiti huu ni kuweka siri kile wanachokizungumza. Hili hufanyika ili kuificha jamii isitambue wanachopanga kukifanya. NkM inasisitiza kufahamu kiini cha kubadili mtindo wa kimatamshi na kimaneno katika kufanya mawasiliano ya kundi linalohusika. Hivyo, mtafiti ameongozwa na nadharia hii katika kutafiti sababu za matumizi ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Sababu hii imeelezwa wakati wa usali na wakati wa mjadala kwa waathirika 25 wa dawa za kulevya waliopo katika nyumba ya kurekebisha tabia na 10 wanaohudhuria kliniki, wazazi 2, walimu 5, askari 3 na wahudumu 10 (watano 5 kutoka katika nyumba za kurekebisha tabia na watano 5 kutoka katika kliniki za waathirika wa dawa za kulevya). Hivyo sababu hii imeelezwa na jumla ya watoa taarifa 55 kati ya 73 ikiwa ni sawa na asilimia 73.3. Watoa taarifa hao wameeleza kuwa licha ya kuhofia kukamatwa au kutuhumiwa na utumiaji wa dawa za kulevya, huwa hawapendi kabisa jamii iwatambue kuwa wanatumia dawa za kulevya na endapo wakibainika basi hujisikia vibaya na ndio maana hufanya mambo yao kwa siri kubwa. Endapo mtu akimwambia ametumia dawa za kulevya hukataa na huwa mkali.

4.4.3 Kuwatia hofu wanajamii

Katika kutafuta kiini cha tatizo la waathirika wa dawa za kulevya kutumia maana fiche katika mazungumzo yao, mtafiti wa utafiti huu amewasaili wahudumu 5, askari 3, walimu 5, wazazi 3, na kufanya mjadala na waathirika 30 wa dawa za kulevya. Jumla ya watoa taarifa hao ni 46 kati ya 73 sawa na asilimia 63 wameeleza kwamba, waathirika wa dawa za kulevya huwa na tabia ya kutumia maneno yenye maana fiche ili kuwatia hofu wanajamii wawaogope na kuwaona ni watu katili wasio na huruma wenye lugha isiyoeleweka. Ifuatayo ni mifano ya mazungumzo yaliyotolewa na waathirika wa dawa za kulevya wakati wa mjadala.

- i. *Olaa! unambwinya sio?*
- ii. *Kausha na utapike.*
- iii. *Cheua cheua fasta.*
- iv. *Haya sambaa sasa.*

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Katika mifano hiyo, muathirika wa dawa za kulevya katumia maneno yenye maana fiche ili aogopewe na aweze kupora mali. Maneno yenyewe ni ‘*unambwinya*’ akimaanisha ‘unasumbua’, ‘*utapike*’ maana yake ‘utoe kila ulichonacho’, ‘*Cheua*’ maana yake ‘toa vitu vyote kwa haraka’, ‘*sambaa*’ maana yake ‘ondoka haraka’ maneno kama haya humtia mtu hofu na kujikuta anafanya kila analoamrisha kufanya. Katika muktadha huu, mtumiaji

wa dawa za kulevya hulazimika kutumia ishara anapozungumza ili yule anayezungumza nae aweze kumuelewa. Kwakuwa mtumiaji wa dawa za kulevya anatumia maana fiche basi huenda kukawa na mtu anasikia mazungumzo hayo lakini akashindwa kutoa msaada kutokana na kushindwa kuelewa maana za maneno yaliyotumika. Hii ni mbinu moja wapo ambayo hupendwa sana kutumiwa na kundi hili linapotaka kufanya uhalifu wa aina yoyote.

4.4.4 Kuogopa unyanyapaa wa wanajamii

Waathirika wa bangi, vidonge na unga hutumia maana fiche kwa sababu ya kuogopa unyanyapaa wa wanajamii. Jumla ya watoa taarifa 33 waliofanyiwa usaili wakiwemo waathirika 28 wa dawa za kulevya (waathirika 11 wa bangi, 4 vidonge na 13 wa unga) Waathirika 21 walitafitiwa kutoka katika nyumba za kurekebishia tabia za walioathirika na dawa za kulevya, 7 kutoka katika kliniki za waathirika wa dawa za kulevya. Pia wahudumu 5 kutoka katika nyumba za kurekebishia tabia walieleza sababu hii na kukamilisha idadi ya watoa taarifa 33 kati ya 73 sawa na asilimia 45.2 ya watoa taarifa wote. NkM imetumika katika uchambuzi wa nukta hii kwa sababu inaeleza sababu kuu za kubadili mtindo wa kimatamshi na maneno ni kuashiria uhusiano na mafungamano ya watu wa jamii fulani. Watoa taarifa hao walieleza kuwa, wanajamii huwa na tabia ya unyanyapaa kwa waathirika wa dawa za kulevya pindi wanapowatambua. Hali hii huwafanya waathirika kujisikia wapweke sana na kukata tamaa ya maisha. Hivyo, ili kujiepusha na unyanyapaa inawabidi kutumia maana fiche ili wanajamii hususani wanafamilia wasiwatilie mashaka na waweze kuendeleza uhusiano wao kama ambavyo NkM inavyoeleza.

4.4.5. Kujitofautisha na wanajamii wengine

Waathirika wa dawa za kulevya hutumia maana fiche ili kujitofautisha na wanajamii wengine. Watoa taarifa 12 wakiwemo walimu 4, wazazi/walezi 7, askari 1 walisailiwa na waathirika 30 wa dawa za kulevya walifanya mjadala ambapo jumla yao ni 42 sawa na asilimia 57.5 walieleza sababu hii. Watoa taarifa hao walieleza kuwa, mtumiaji wa dawa za kulevya kabla ya kuanza kutumia dawa hizo hutumia lugha ya kawaida inayoeleweka na jamii nzima. Anapoanza kutumia dawa za kulevya hujikuta anaiga mtindo wa matamshi na maneno mapya wakati wa mawasiliano na waathirika wenzake kama ambavyo NkM inavyoeleza; binaadamu hujitahidi kuzungumza lugha au kuiga namna fulani ya matamshi ya lugha na maneno mapya kutoka kwa msikilizaji wake ili aweze kukidhi haja ya mawasiliano na kukubalika katika jamii ya watumiaji wa dawa za kulevya. Nukta hii inadhihirisha kuwa; waathirika wa dawa za kulevya huwa na rejesta yao ambayo huitumia baina yao.

Jadweli lifuatalo linaonesha sababu za matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya ili kubainisha uzito wake katika asilimia

Jadweli na: 4.16. Matokeo ya sababu za matumizi ya maana fiche

Na	Sababu za Matumizi Ya Maana Fiche	Idadi ya Watoa Taarifa	Asilimia	Nafasi
1	Sababu za Kiusalama	68	93.2	1
2	Kuweka Siri	55	73	2
3	Kuwatia Hofu Wanajamii	46	63	3
4	Kujitofautisha na Wanajamii Wengine	42	57.5	4
5	Kuogopa Unyanyapaa wa Wanajamii	33	45.2	5

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Matokeo yanaonesha kuwa sababu kuu ya utumiaji wa maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya ni usalama. Wasailiwa wote wameitaja na kuielezea sababu hii isipokuwa waathirika wa maskani tu ambao hawakupata fursa ya kusailiwa wala kufanyiwa mjadala. Wao walitafitiwa kwa njia ya ushuhudiaji kama ilivyokwishaelezwa. Sababu ya kiusalama ilielezwa na watoa taarifa 68 sawa na asilimia 93. Sababu hii ilifuatiwa na ile ya kuweka siri ambayo ilielezwa na wasailiwa 55 kati ya 73 sawa na asilimia 73. Sabababu ya tatu ni kuwatia hofu wananchi ambayo imeelezwa na watoa taarifa 46 sawa na asilimia 63 ikifuatiwa na kujitofautisha na wanajamii wengine ambayo imeungwa mkono na watoa taarifa 42 sawa na asilimia 57.5. Hoja ya mwisho ni

kuogopa unyanyapaa wa wanajamii ambayo imeelezwa na watoa taarifa 33 sawa na asilimia 45.2.

4.5. Athari za matumizi ya maana fiche

Lengo la nne la utafiti huu ni kutathmini athari za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la nne lililouliza; Ni zipi athari za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar? Watoa taarifa walisailiwa pia wakafanya mjadala na kueleza athari mbalimbali za matumizi ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Kulingana na NkM kupitia mhimili wa pili inaeleza kuwa, katika jamii mawasiliano huathiriwa na mazungumzo ambayo ndiyo hutoa tafsiri na kuuhukumu ujumbe uliobebwa katika mazungumzo hayo. Hivyo kwa msaada wa mhimili huu wa NkM matumizi ya maneno yenye maana fiche yamebainika kuwa na athari mbalimbali katika jamii. Athari hizo zipo hasi na athari chanya. Kwa kuanzia na athari hasi, data zinaonesha athari sita za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar kama ifuatavyo:

4.5.1. Kuharibu lugha ya kiswahili

Utumiaji wa maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya hupelekea kuharibu lugha ya Kiswahili. Athari hii imeelezwa na watoa taarifa 56 wakiwemo walimu 10, wazazi/walezi 10, skari 3, wahudumu 10 na waathirika wa dawa za kulevya 23 hivyo kufikia asilimia 76.7 ya watoa taarifa wote kama inavyobainishwa katika

jadwali 4.18. watoa taarifa wameeleza kuwa, ili lugha ikue inapaswa kutumiwa na wanajamii. Endapo lugha hiyo itatumiwa na kikundi fulani tena kwa kuficha maana kwa sababu zao binafsi, husababisha kuharibu lugha hiyo. Watoa taarifa walieleza haya wakati wa usaili pia walipokuwa wakifanya mjadala katika makundi yao. Utafiti umebaini kuwa waathirika wa dawa za kulevya hupendelea zaidi kutumia maneno yenye maana fiche kuliko yale yenye maana ya msingi. Wakati mwingine hubuni maneno yasiyojulikana na wanajamii wengine na kuyatumia badala ya maneno sanifu. Hali hii husababisha kuharibu lugha ya Kiswahili. Mifano mbalimbali ya maneno yenye maana fiche yanayoharibu lugha ya Kiswahili ambayo hutumiwa na waathirika wa dawa za kulevya imeoneshwa katika jadwali na. 4.17

Jadwali Na 4.17: Maneno yenye maana fiche yanavyoharibu lugha

Na	Msamiati	Maana ya Msingi	Maana Fiche
1	<i>Wazee</i>	Lakabu ya heshima ya mwanamme.	Askari wa kupambana na dawa za kulevya.
2	<i>Sembe</i>	Unga unaotokana na mahindi yaliyosagwa.	Unga (dawa ya kulevya)
3	<i>Mwana</i>	Mtoto wa mtu au mnyama	Mteja wa dawa za kulevya
4	<i>Wadudu</i>	Ni viumbe hai wenye gimba lililogawanyika sehemu tatu bayana: kichwa, kifua na fumbatio.	Askari
5	<i>Farasi</i>	Mnyama mkubwa wa kufuga anaefanana na punda mwenye manyoa shingoni na mkia wa singa	Gari la polisi
6	<i>Mzungu</i>	Mtu mwenye asili na mwenyeji wa Ulaya	Muuzaji unga (dawa za kulevya)
7	<i>Mchawi</i>	Mtu anaetumia mazingaombwe kuwadhuru wengine.	Askari
8	<i>Sanda</i>	Kitambaa cheupe anachovikwa maiti wa kiislamu kwa utaratibu maalumu na kuzikwa nacho	Karatasi ya kusokotea bangi kwa ajili ya kuvuta.

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Katika mifano hiyo tunaona kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno ya kawaida yakiwa na maana fiche na kusababisha kuharibu lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu wanajamii hususani watoto hushindwa kutambua maana halisi ya neno. NkM inaeleza kuwa; mawasiliano yasiyo wima mara nyingi hujitokeza pale ambapo mzungumzaji fulani anapozungumza na watu wa rika la vijana na ikabidi ajilazimishe kuimarisha lugha ili aweze kukidhi haja ya kufanya mawasiliano yanayopendeza zaidi baina yao. Hivyo, mkazo wa lugha hujitokeza katika muktadha wa utambulisho. Athari hii

imeelezwa wakati wa usaili wa walimu 10, wazazi/ walezi 10, askari 3, wahudumu 10 pamoja na waathirika wa dawa za kulevya 23 ambao walifanya mijadala katika makundi yao. Jadweli na. 4.18 linabainisha watoa taarifa walioelezea nukta hii.

Jadweli Na. 4.18 Muhtasari wa watoa taarifa walioelezea namna lugha inavyoathirika

Na.	Watoa taarifa	Adadi	Asilimia
1	Walimu	10	17.9
2	Wazazi/walezi	10	17.9
3	Askari	3	5.3
4	Wahudumu	10	17.9
5	Waathirika	23	41
	JUMLA	56	100

4.4.2 Mwendelezo wa uingizwaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya

Utumiaji wa maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya hupelekea mwendelezo wa uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Hii ni athari hasi ambayo hupelekea jamii kuathirika kwa dawa za kulevya kwa kiwango cha juu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, watumiaji wa dawa za kulevya huficha maana kwa lengo la kuficha shughuli zao wanazozifanya zisijulikane na mtu yeyote asiyekuwa miongoni mwao. Kwakuwa usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya ni kinyume cha sheria, shughuli hizo hufanywa kwa siri kubwa. Watoa taarifa 21 (wahudumu 8, wazazi 4,

walimu 7, askari 2) walifanyiwa usaili na waathirika 5 walifanya mjadala. Hivyo, jumla ya watoa taarifa 26 sawa na asilimia 35.6 wamedokeza jambo hili wakati wa ukusanyaji data. Tuangalie mifano ifuatayo iliyotolewa na waathirika waliohudhuria kliniki ya waathirika wa dawa za kulevya katika Hospitali ya Mwembeladu:

- a) Mwathirika 1: *“Muda wa ibada sasa bilali keshakimu sala”*.
- b) Mwathirika 2: *“ok, tusepe”*
- c) Mwathirika 3: *“nendeni, mimi nakimbilia mtambo wa kwanza”*
- d) Mwathirika 4: *“Leo ni chapori tu, niko mabovu”*

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Katika hali ya kawaida huwezi kubaini iwapo wazungumzaji wa hapo juu, wanakwenda maskani badala yake utadhani wanaelekea msikitini. Kitakachokushangaza ni kwanini maneno hayo yanazungumzwa muda ambao si wa sala za jamaa. Utajiuliza wanakwenda kusali sala gani na muda bado au umeshapita. Katika mfano c) mwathirika wa 3 anakusudia kusema anataka pombe (gongo) ambayo haijatiwa maji. Kwa asiyekuwa muathirika wa dawa za kulevya anaweza kudhani mwathirika huyo anahitaji maji ya kunywa. Vilevile katika mfano d) mwathirika wa dawa za kulevya anaeleza kuwa, hana pesa, hivyo watakunywa pombe ya porini.

Ufichaji huu wa maana huchochea uingizwaji na usambazwaji wa dawa za kulevya kutokana na kuwa huru kufanya shughuli zao pasi na kukamatwa wala kutuhumiwa. Watumiaji wa dawa za kulevya huweza kupeana taarifa mbalimbali pasi na kufahamika na

mtu asiyekuwa miongoni mwao. Hali hii huwapa uhuru wa kuendeleza biashara hii haramu. Hii inadhihirisha kuwa binadamu hujitahidi kuzungumza lugha au kuiga namna fulani ya matamshi ya lugha na maneno mapya ili aweze kukidhi haja ya mawasiliano kama ambavyo Nadharia ya Kidhi ya Mawasiliano inavyosisitiza.

4.5.3 Huathiri harakati za mapambano dhidi ya dawa za kulevya

Pamoja na juhudi kubwa inayochukuliwa na serikali pamoja na taasisi zake maalumu zilizoundwa kupambana na dawa za kulevya, bado juhudi hizo hazijafikia katika mafanikio ya kuridhisha. Hii ni kwa sababu jamii pamoja na taasisi zinazopambana na dawa hizo hushindwa kuwatambua na kuwakamata watumiaji na wasambazaji wa dawa hizo kwa sababu ya kutoelewa kile wanachokizungumza. Mfano, huenda muuzaji wa dawa za kulevya na mteja wake wanaweza wakawa wanauziana au wanapanga miadi ya kukutana kwa ajili ya kuuziana dawa hizo lakini kutokana na kuficha maana, huenda wasieleweke kwa wanajamii na hata askari wanaopambana na dawa hizo. Mfano:

- a) *Vipi pusha yupo?*
- b) *Nipimie sembe.*
- c) *Mazeee mbona naona pana doriani hapa?*
- d) *Oyaa wazee na farasiii*
- e) *Yakumwaga mwana*

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Katika mfano (a), katika hali ya kawaida unaweza ukadhani kuwa ‘*pusha*’ ni jina la mtu au mtu anayesaidia watu wengine (pusher) lakini kumbe anaauliziwa ni muuza unga, vidonge au charas. Katika mfano (b), utajua anahitaji unga wa sembe kumbe anaulizia unga (dawa ya kulevya). Vilevile, mfano (c), unaweza kufahamu kuwa, doriani linalozungumziwa ni tunda ilhali ni mtu anayetiliwa mashaka kuwa ni mpelelezi na hapo utaona kila mmoja ananyanyua uso na kuangaza huku na kule kuona kama kuna mtu wasiemtambua. Pia mfano (d), ‘*wazee*’ waliokusudiwa hapo ni askari na ‘*farasi*’ ni gari la askari na katika mfano (e) mwanajamii ambaye si muathirika wa dawa za kulevya anaweza kufahamu kuwa ‘*Yakumwaga*’ ni kitu ambacho hakifai kwa matumizi kumbe maana iliyokusudiwa ni ‘nyingi yakutosha’.

Hivyo, NkM inaelezea sababu za kubadili mtindo wa kimatamshi na kimaneno katika kufanya mawasiliano katika jamii husika kuwa ni kukidhi haja ya mawasiliano. Waathirika wa dawa za kulevya hutumia maana fiche za maneno ili kukidhi mawasiliano baina yao tu kama ambavyo NkM imeelekeza. NkM inadhihirisha kuwa, utumiaji wa maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya huathiri kwa kiasi kikubwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini. Imethibitika kwamba, taasisi zinazopambana na dawa za kulevya wakati mwingine hupata ugumu kuwakamata waathirika wa dawa za kulevya kutokana na kutofahamu kile wanachozungumza. Haya yameelezwa na watoa taarifa waliofanyiwa usaili; askari 3, wahudumu 10, walimu 8 na wazazi/ walezi 7, jumla 28 sawa na asilimia 38.4. Hivyo, waathirika wa dawa za kulevya hulazimika kubadili

maneno au kubuni maneno mapya yenye maana fiche ili kukidhi mawasiliano kama ambavyo Nadharia Kidhi ya Mawasiliano inavyotuelekeza.

Jadweli Na. 19: Muhtasari wa Watoa Taarifa Kuhusu Athari Katika Mapambano ya Dawa za Kulevyo

Na	Watoa Taarifa	Idadi	Asilimia
1	Askari	3	10.7
2	Wahudumu	10	35.7
3	Walimu	8	28.6
4	Wazazi/walezi	7	25
	JUMLA	28	38.4

4.5.4 Ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevyo

Data zimeonesha kuwa, matumizi ya maana fiche husababisha wanajamii hususani vijana kushawishika na kujiingiza katika kundi la watumiaji wa dawa za kulevyo. Kila mwanadamu ana matamano yake, hivyo wapo baadhi ya watu huvutiwa na lugha ya waathirika wa dawa za kulevyo na kuona kuwa ni lugha ya kijanja kwa sababu inasiri. Vilevile kuna majina ambayo hutumiwa na waathirika wa dawa za kulevyo kwa ajili ya kuwadhihaki wale wasiotumia. Hali hii huwafanya baadhi yao hususani vijana kujisikia vibaya na kuamua kujiingiza katika kundi hilo ili waweze kuwa miongoni mwao na kufuta

jina hilo. Mfano wa majina wanayoitwa wale wasiotumia dawa za kulevya ambayo huwadhalilisha yameorodheshwa katika jadweli na. 4.18.

Jadweli Na. 4.20: Majina yanayowadhihaki vijana wasiotumia dawa za kulevya

Jina	Maana ya Msingi	Maana Fiche
<i>Mwari</i>	Msichana ambae amebaleghe lakini hajaolewa.	mtu asiyevuta bangi
<i>Boga</i>	Tunda kubwa lenye umbo la mviringo, maganda magumu, nyama rangi ya njanona kokwa nyingi, la mmea jamii ya mtango, linaloliwa baada ya kupikwa.	mtu asiyetumia unga
<i>Mdananda</i>	Maneno ya kubuni.	Mtu asiyetumia dawa yoyote ya kulevya likimfananisha na mwanaume shoga
<i>Kumbi</i>	Ganda la nje la nazi au dafu.	Mtu asiyekunywa pombe

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020).

Maneno hayo (katika jadweli na. 4.17) humfanya mtu ajisikie vibaya na ili kulinda hadhi na heshima yake hujikuta ameshawishika na kuingia katika utumiaji wa dawa za kulevya. Watoa taarifa walieleza baadhi ya mifano ya sentensi zenye maneno yenye maana fiche ambazo huweza kupelekea wanajamii kushawishika kujiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya. Mfano wa sentensi iliyotolea na muathirika wa dawa za kulevya anayeishi katika nyumba ya kurekebisha tabia ya waathirika wa dawa za kulevya: “*ukipiga pafu mbili tatu tayari ushapendeza no stress unatuliaa kuskilizia stimu*”. Watoa taarifa wameeleza kuwa, maneno kama haya huweza kumshawishi mtu na kumpelekea kujaribu kutumia dawa hizo

ili aone starehe yake ajue hiyo stimu ni ipi au pengine aweze kupunguza msongo wa mawazo kumbe atakapoanza tu itakuwa ni vigumu sana kuacha.

Athari hii imeelezwa na waathirika 21 ambao wamefanya mijadala baina yao (waathirika 14 ni kutoka katika nyumba za kurekebisha tabia za waathirika wa dawa za kulevya na 7 kutoka katika kliniki za waathirika wa dawa za kulevya). Watoa taarifa hawa wamethibitisha kuwa walijiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya baada ya kushawishika; ama kwa kuogopa fedheha ya kuitwa majina mabaya au kwa kuvutiwa na lugha ya waathirika wa dawa za kulevya na kuamua kujaribu. Matokeo yake baada ya kujaribu tu wakashindwa kabisa kuacha mpaka pale walipokwenda kuishi katika nyumba za kurekebisha tabia na kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kupata huduma sahihi. Hivyo, matokeo yameonesha kuwa, lugha huweza kumfanya mtu kuiga au kijiingiza katika kundi fulani na hata kuiga matendo fulani, iwe kwa kukusudia au kwa kutokusudia ili waweze kukubalika. Nadhari Kidhi ya Mawasiliano inathibitisha hayo katika mhimili wake kwamba wanaadamu katika maisha yao hujaribu kuibua aina fulani ya wigo ndani ya matamshi kutoka kwa mtu mwingine, ilimradi aweze kukidhi kiu yake ya kufanya mawasiliano baina yao na mtu mwingine.

4.5.5 Kuathiri mawasiliano baina ya wahudumu na waathirika wa dawa za kulevya

Utumiaji wa maana fiche za maneno huathiri mawasiliano kati ya mwathirika na muhudumu hasa kwa wahudumu wa kliniki za waathirika wa dawa za kulevya. Athari hii huwakumba zaidi wahudumu wa kliniki hususani wahudumu wapya (ambao bado

hawayajui maneno yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya) wanapokutana na waathirika wapya (ambao ndo wanaanza kupatiwa huduma). Kwa mfano:

Mwathirika: *“nilipewa dawa hizi lakini zinambwinya kinoma”*

Muhudumu: *“zinambwinya ndo zinafanya nini?”*

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Katika mfano huo, mwathirika wa dawa za kulevya alikusudia kusema *‘nilipewa dawa hizi lakini zinanisumbua sana’*. *Zinambwinya* ni neno lenye maana fiche ambalo limesababisha muhudumu kutoelewa kilichozungumzwa na mwathirika. Athari hii imeelezwa wakati wa usaili wa wahudumu; wahudumu 10 wa kliniki za waathirika wa dawa za kulevya na 5 kutoka katika nyumba za kurekebisha tabia. Jumla ni watoa taarifa 15 sawa na asilimia 20.5. Wasailiwa hao wameeleza kuwa, wakati mwingine hushindwa kufahamu kile kinachozungumzwa na waathirika wa dawa za kulevya kutokana na utumiaji wa MyK na hata kutumia maana fiche za msamiati. NkM inaeleza kuwa, mwanadamu wakati mwingine humbidi kufanya wigo wa kimaneno au vipengele vingine vya lugha kutoka kwa mtu mwingine ambaye anafanya nae mazungumzo ili kutimiza lengo la mawasiliano. Hivyo, ili mawasiliano yaweze kukamilika inamlazimu muhudumu mpya kujifunza baadhi ya maneno yenye maana fiche yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya (maneno wanayotumia mara kwa mara) kama nadharia ya kidhi ya mawasiliano inavyoongoza.

4.5.6 Kuharibu utamaduni wa jamii

Data za utafiti zinaonesha kuwa waathirika wa dawa za kulevya wanapotumia maana fiche katika mawasiliano husababisha utamaduni wa jamii kuporomoka. Kwakuwa lugha ni sehemu ya utamaduni, inapaswa itumike kwa mujibu wa mila na desturi za wanajamii. Kupitia utafiti huu, imethibitika kuwa, utumiaji wa maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya huathiri lugha ya Kiswahili ambayo ni sehemu ya utamaduni wa Mswahili kama ilivyoelezwa. NkM inasisitiza kwamba, wanaadamu katika maisha yao hujaribu kuibua aina fulani ya wigo ndani ya matamshi kutoka kwa mtu mwingine, ilimradi aweze kukidhi kiu yake ya kufanya mawasiliano baina yake na mtu mwingine. Mhimili huu wa NkM umeakisi matokeo ya utafiti ambayo yamebaini kuwa, wanajamii hususani vijana na watoto huchanganya mitindo ya lugha ya Kiswahili Sanifu na mitindo ya lugha inayoibuliwa na waathirika wa dawa za kulevya hususani katika kipengele cha semantiki na fonolojia na hivyo kuharibu utamaduni.

Mfano wa msamiati: *mabovu, mazuri, Pafu, Jojiwea, Maji, Wazee, Njaa kali, Wachawi, Wadudu, Adimu, Sanda, Nguo, Majani, Doriani, Farasi, Mwari, Nyuki na Mtambo*. Hayo ni maneno sanifu ya lugha ya Kiswahili lakini yanapotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya hutumiwa kwa maana tofauti kama ilivyokwisha elezwa na kuharibu utamaduni wa Waswahili. Hoja hii imeelezwa na jumla ya watoa taarifa kutoka makundi mbalimbali. Jumla yao ni 61 sawa na asilimia 100 ya watoa taarifa wote.

Jadweli Na. 4.21: Huharibu utamaduni wa jamii

Na.	Kundi	Idadi	Asilimia
1	Waathirika	24	39.3
2	Kliniki	4	6.6
3	Maskani	3	4.9
4	Wahudumu	8	13.1
5	Askari	3	4.9
6	Walimu	10	16.4
7	Wazazi /Walezi	9	14.8
	Jumla	61	100

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020).

4.4.7 Kukuza lugha

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, baadhi ya maneno yenye maana fiche huweza kufichuliwa maana yake na kuanza kutumiwa na wanajamii wote. Kwakuwa wanajamii huwa na tabia ya kuiga maneno kama ambavyo NkM inasisitiza kwamba, wanaadamu katika maisha yao hujaribu kuibua aina fulani ya wigo ndani ya matamshi kutoka kwa mtu mwingine, ilimradi aweze kukidhi kiu yake ya kufanya mawasiliano baina yake na mtu mwingine. Wanajamii huiga maneno yanaobuniwa na waathirika wa dawa za kulevya na

kuyatumia ama kwa kutambua maana yake au kwa kutotambua maana ya maneno hayo. Maneno hayo yanapotumiwa kwa muda mrefu, huweza kusanifishwa na kuwa sehemu ya msamiati wa lugha ya Kiswahili. Hivyo hupata kibali cha kutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii zilizo rasmi. Haya yameelezwa na walimu 5 wa skuli teule ambao ni sawa na asilimia 6.8. Giles amefafanua kuwa sababu kuu ya kubadili mtindo wa matamshi ya maneno ni kuonesha makubaliano na uhusiano kwa watu wengine. Hali hii huwafanya watu wengi kujihisi kuwa wanahusiana kama Nadharia kidhi ya Mawasiliano inavyotuongoza. Jadwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa athari za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Jadweli Na. 4.22 Athari za Maana Fiche za Maneno

N	Athari za maana fiche	Watoataarifa	Asilimia	Nafasi
1	Kuharibu lugha ya Kiswahili	56	76.7	2
2	Mwendelezo wa Uingizwaji, Usambazaji na Utumiaji wa Dawa za Kulevya	26	35.6	5
3	Huathiri Harakati za Mapambano Dhidi ya Dawa Hizo	28	38.4	4
4	Ongezeko la Watumiaji wa Dawa za Kulevya	41	56.2	3
5	Huathiri Mawasiliano Baina ya Wahudumu na Waathirika wa Dawa za Kulevya	15	20.5	6
6	Huharibu Utamaduni wa Jamii	61	83.6	1
7	Kukuza Lugha.	5	6.8	7

Chanzo: Data kutoka uwandani (2020)

Kwa ujumla, matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar yameonekana kuwa na athari kwa jamii ya Wazanzibari. Matokeo ya utafiti yamethibitisha kuwa athari kubwa ya matumizi ya maana fiche ni kuharibu utamaduni wa jamii ya Wazanzibari. Haya yameelezwa na watoa taarifa 61 kati

ya 73 sawa na asilimia 83.6, ikifuatiwa na kuharibu lugha ya Kiswahili ambayo imeelezwa na watoa taarifa 56 kati ya 73 sawa na asilimia 76.2. Athari iliyoelezwa na watoa taarifa wachache zaidi ni kukuza lugha ya Kiswahili ambayo imeelezwa na watoa taarifa 5 kati ya 73 sawa na asilimia 6.8. Haya yote yameoneshwa kwa uwazi katika jadweli na. 4.19.

4.6. Muhtasari wa sura

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu za usaili, ushuhudiaji na mjadala wa kundi lengwa. Uwasilishaji huo umezingatia malengo ya utafiti na umeongozwa na mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Aidha, Nadharia ya Maana ni Matumizi na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano ndizo zilizoongoza katika kuchanganuzi wa data. Mtafiti alifanikiwa kukusanya maneno yaliyoibua maana mpya kwa waathirika wa dawa za kulevya. Pia maana fiche hizo zimeelezwa katika sura hii. Vilevile mtafiti amechambua sababu za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Mwisho, ametoa tathmini ya athari ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5. 1 Utangulizi

Sura hii ya tano ambayo ndiyo ya mwisho, inahitimisha utafiti huu unaohusu Maana Fiche ya Maneno Yanayotumiwa na Waathirika wa Dawa za Kulevya. Sura imegawika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inaeleza muhtasari wa matokeo ya utafiti. Sehemu ya pili inaeleza hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu inatoa mapendekezo mbalimbali ya tafiti zijazo.

5.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti.

Utafiti huu ulichunguza maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Mtafiti amechambua na kubainisha matokeo ya utafiti kwa kila lengo lililokusudiwa. Kwa ujumla tasnifu hii imejengwa kwa sura tano zenye vipengele mbalimbali. Katika sura ya nne data zimewasilishwa na kuchanganuliwa kwa makini na hatimaye matokeo ya kila hatua kuoneshwa. Uchambuzi huo umeongozwa na Nadharia ya Maana ni Matumizi na Nadharia Kidhi ya Mawasiliano kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa katika sura ya nne, katika sehemu hii mtafiti anabainisha muhtasari wa matokeo ya utafiti wake kwa mujibu wa malengo aliyojiwekea;

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la kwanza lililokusudia kutaka kubainisha maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Mtafiti alikusanya maneno mengi kabla ya kuyafanyia upembuzi. Kutoka katika orodha hiyo ya maneno, utafiti ulibaini maneno mia moja na sita (106) yaliyokuwa na maana fiche. Maneno hayo yapo katika makundi makuu matatu ya lugha; maneno yenye asili ya lugha ya Kiswahili, maneno yenye asili ya lugha za kigeni na MyK yasiyofungamana na lugha yoyote.

Imebainika kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi kundi la maneno ya lugha ya Kiswahili. Kundi hilo lilikuwa na maneno sitini na tano (65) kati ya 106 yaliyokusanywa ambayo ni sawa na asilimia 61.3. Kundi la pili lililofuatia ni lile la MyK ambalo lilikuwa na jumla ya maneno ishirini na moja (21) kati ya 106 sawa na asilimia 19.8. Kwa upande mwingine kundi la LgzK ndilo lililobainika kuwa na idadi ndogo zaidi ya maneno kwa kuwa na jumla ya maneno ishirini (20) kati ya 106 sawa na asilimia 18.9.

Katika makundi haya matatu ya lugha, imebainika kuwa, katika kundi la maneno yenye asili ya lugha ya Kiswahili kuna miundo tofauti ya maneno, aina za maneno na matumizi ya virai. Matokeo ya utafiti yamebaini miundo mitatu ya maneno yenye asili ya lugha ya Kiswahili yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya;

- Muundo wa maneno ambatani ya maneno matatu
- Muundo wa maneno ambatani ya maneno mawili
- Muundo wa neno moja

Katika aina za maneno ya Kiswahili matokeo yanaonesha kuwa waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi nomino kuliko aina nyingine za maneno. Kwa upande mwingine

imebainika matumizi madogo ya vivumishi na hakukuwa na aina nyingine za msamiti uliobainika. Utafiti umebaini pia waathirika wa dawa za kulevya hutumia zaidi virai vilivyoundwa kwa maneno mawili kuliko vile vilivyoundwa kwa maneno matatu.

Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha miundo tafauti ya MyK kama inavyooneshwa hapo chini.

- MyK ambayo yameundwa kwa silabi moja,
- MyK ambayo yameundwa kwa silabi mbili,
- MyK ambayo yameundwa kwa silabi tatu; na
- MyK ambayo yameundwa kwa silabi nne.

Imebainika kuwa, silabi zilizomo katika MyK zimeundwa kwa kufuata utaratibu wa miundo ya silabi za Kiswahili. Matokeo yanaonesha kuwa, MyK huundwa kwa silabi mbili, tatu au nne ambapo jumla ya MyK kumi na moja (11) sawa na asilimia 52.4 yameundwa kwa silabi tatu. Kundi linalofuatia kwa wingi wa MyK ni lile lenye silabi nne ndani yake. Katika kundi hili, Jumla ya maneno saba (7) sawa na asilimia 33 yamebainika. Aidha, kundi la MyK yenye silabi mbili limebainika kuwa na idadi ndogo ambalo lina maneno matatu (3) sawa na asilimia 14.3.

Pamoja na hayo, matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa, waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar hutumia zaidi MyK yenye maana fiche yaliyoundwa kwa silabi huru. MyK 15 sawa na asilimia 71.4 yamebainika kuwa yameundwa kwa silabi huru na maneno sita 6 ya kubuni ambayo ni sawa na asilimia 28.6 yameundwa kwa mchanganyiko wa silabi huru na

silabi funge. Pamoja na aina za silabi zilizobainika, matokeo ya utafiti pia yamebaini miundo ya silabi ambapo idadi kubwa ya MyK yamebainika kuwa yameundwa kwa kutumia muundo wa konsonanti na irabu. Jumla ya maneno saba (7) ya kubuni sawa na asilimia 33 yameundwa kwa kufuata muundo huo. Muundo wa pili wa silabi uliobainika kutumika kubuni maneno ni muundo wa konsonanti pekee. Muundo huo umebainika katika maneno sita (6) ya kubuni sawa na asilimia 28.6. Muundo mwingine wa silabi katika MyK ni muundo wa irabu pekee. Muundo huu umebainika katika maneno manne (4) sawa na asilimia 19. Vilevile muundo wa konsonanti mbili na irabu moja umebainika kutumika katika baadhi ya maneno. Jumla ya maneno matatu (3) ya kubuni sawa na asilimia 14.3 yameundwa kwa kutumia muundo huo wa silabi.

Sambamba na hayo, utafiti pia umebaini muundo wa silabi wa konsonanti tatu na irabu. Muundo huu hutumiwa kwa kiasi kidogo sana katika kubuni maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Neno moja limebainika kuundwa kwa kutumia muundo huo ambalo ni sawa na asilimia 4.7.

Kwa upande wa maneno yenye asili ya LgzK, matokeo yanaonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya hutumia lugha tano za kigeni (Kiingereza, Kiarabu, Kifaransa, Kijerumani na Kihispania). Jumla ya maneno 20 kati ya 106 ambayo ni sawa na asilimia 18.9 yamebainika kuwa na asili ya LgzK ambayo mara nyingi hutamkwa kama maneno ya lugha ya Kiswahili. Katika kutafiti Matamshi ya maneno yenye asili ya LgzK yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya, matokeo ya utafiti yamebaini ufuatishwaji wa sheria za

matamshi ya lugha ya Kiswahili wakati wa kutamka maneno yenye asili ya LgzK. Sheria ilizobainika ni uambishaji wa irabu mwishoni mwa maneno yanayoishia na konsonanti.

Utafiti pia umebaini aina tatu za maneno yenye asili ya LgzK; nomino, vivumishi na vitenzi. Matokeo ya utafiti yanaonesha idadi kubwa ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya ambayo asili yake ni LgzK ni nomino. Jumla ya nomino (8) sawa na asilimia 40 zimebainika. Vivumishi pia vimebainika katika utafiti huu. jumla ya maneno matano (5) sawa na asilimia 25 yalikuwa katika kundi la vivumishi. Kwa upande mwingine idadi ndogo ya vitenzi ilibainika. Vitenzi vilikuwa 3 sawa na asilimia 15 ya maneno yote yenye asili ya LgzK.

Lengo la pili la utafiti huu ni kufafanua maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la pili lililouliza: Ni zipi maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar? Matokeo ya utafiti yameonesha; waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno ya kawaida ambayo maana yake ya msingi huwa inafahamika kwa wanajamii wote. Hata hivyo, wao (waathirika wa dawa za kulevya) kuyabebesha maneno hayo maana mpya (fiche). Sambamba na hayo, waathirika wa dawa za kulevya hubuni maneno mapya ambayo hayajulikani na wanajamii na kuyatumia kwa lengo la kukidhi mawasiliano baina yao. Si hayo tu, waathirika wa dawa za kulevya pia hutumia maneno ya LgzK ili kuficha maana waliyokusudia. Matokeo yanaonesha kuwa, waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar hutumia maana fiche wanapobainisha aina za dawa za kulevya, vipimo vya dawa

za kulevya, vifungashio vya dawa za kulevya, maana fiche zinazohusu taasisi zinazopambana na dawa za kulevya, maneno yanayobainisha majina ya wauzaji wa dawa za kulevya pamoja na maneno yanayotumika kuwadhihaki vijana wasiotumia dawa za kulevya.

Kwa kuanzia na aina za dawa za kulevya, matokeo ya utafiti yamebaini kwamba, dawa moja ya kulevya imepewa majina zaidi ya moja yenye maana fiche. Hii ni kwa sababu ya kumrahisishia muuzaji wa dawa za kulevya kumtambua mteja wake na eneo analotokea.

Vielevile, matokeo ya utafiti yamebaini kuwa; waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno ya kawaida katika kubainisha vifungashio vinavyotumika kufungia au kusokotea dawa ya kulevya kwa ajili ya matumizi. Maneno wanayotumia ni yale yanayoeleweka na wanajamii. Ingawa hivyo, wao huyatumia kwa maana tofauti na ile ya msingi. Vifungashio hivyo hutumika kusokotea bangi kama ilivyoielezwa.

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yamebaini kuwa, waathirika wa dawa za kulevya wanatambua kuwa utumiaji wa dawa za kulevya ni kinyume cha sheria na wanatambuwa kuwepo wa taasisi na vyombo mbalimbali vinavyopambana na dawa za kulevya. Hii ndio sababu inayowafanya watumie maana fiche wanapozungumzia kuhusu vyombo na taasisi hizo. Hivyo, watumiaji wa lugha wana nafasi kubwa katika upatikanaji wa maana ya maneno. Ni vigumu sana kubaini maana ya maneno pasi na kumuhusisha mtumiaji au watumiaji kama Nadharia ya Maana ni Matumizi inavyoeleza.

Matokeo ya utafiti katika lengo la tatu la utafiti huu ambalo ni kujadili sababu za matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali lililouliza; ni zipi sababu za matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar? Watoa taarifa wameweza kueleza sababu tano za utumiaji wa maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya. Sababu hizo ni;

- Sababu za kiusalama,
- Kuweka siri,
- Kuwatia hofu wanajamii,
- Kuogopa unyanyapaa wa wanajamii na
- Kujitofautisha na wanajamii wengine.

Lengo la nne la utafiti huu ni kutathmini athari za maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar. Lengo hili liliongozwa na swali la nne lililouliza; Ni zipi athari za matumizi ya maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar? Matokeo ya utafiti yamebaini athari saba (7) za matumizi ya maana fiche ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya;

- Kuharibu lugha ya Kiswahili,
- Mwendelezo wa uingizwaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya,
- Huathiri harakati za mapambano dhidi ya dawa za kulevya,
- Hupelekea watu kushawishika na kujiingiza katika kundi hilo,

- Kutokuelewana baina ya wahudumu wa waathirika wa dawa za kulevya na
- Kuogopa unyanyapaa kutoka katika jamii zao.

5.3 Mapendekezo

Kwa kawaida utafiti wowote wa kitaaluma huwa na dhamira ya kutoa matokeo ya kitaaluma katika uwanja uliofanyiwa kazi. Utafiti huu umetowa mchango wa kitaaluma katika uga wa lughawiya, hususan kipengele cha semantiki. Aidha, taasisi zinazopambana na dawa za zinategemewa kunufaika kwa kiasi kikubwa na matokeo ya utafiti huu. Kutokana na mchango wa utafiti huu, mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo;

5.3.1 Mapendekezo ya jumla

Jamii na wadau wa lugha wazidi kuhamasisha utumiaji wa maana za msingi katika mawasiliano ili kuepuka kuiathiri lugha ya Kiswahili kama ambavyo imekwisha elezwa katika sura ya nne (4.4). Vile vile wadau wa lugha wawatembelee waathirika wa dawa za kulevya waliopo katika nyumba za kurekebisha tabia na wanaohudhuria kliniki za waathirika wa dawa za kulevya ili kuwashajihisha kutumia maana sahihi za maneno na wao kuwa mabalozi kwa waathirika waliopo mitaani ili kuepusha upotoshaji wa maana kwa wanajamii wengine.

5.3.2 Mapendekezo ya tafiti fuatizi

Sambamba na hayo, utafiti unapendekeza tafiti zijazo ziangazie katika matumizi ya lugha ya waathirika wa dawa za kulevya kwa kuchambua vipengele vya kifonolojia, mofolojia

na sintaksia ili kuona kama kuna tofauti kati ya kundi hili na kundi jingine. Hivyo, utafiti huu ni chachu ya kutoa fursa ya kufanya tafiti nyingine zinazohusu mada kama hii.

5.4 Hitimisho

Katika utafiti huu imebainika kwamba, waathirika wa dawa za kulevya hutumia maneno yenye maana fiche kwa sababu mbalimbali kama zilivyobainishwa katika sura ya nne namba 4.3. Matumizi hayo ya maneno yenye maana fiche yana athari mbalimbali kwa lugha, jamii na taifa kwa ujumla. Athari hizo zimebainishwa katika sura ya nne nambari 4.4 ya tasnifu hii.

MAREJELEO

Akmajian, A. Demers, R. Farmer, A. & Harnish, R. (2010). *Linguistics: An introduction to language and communication*. MIT Press.

Ame, M. (2013). *Mama Shein asaidia 'soba'*. Imepakuliwa kutoka <http://www.zanzinews.com/2013/07/mama-shein-asaidia-sober-house.html> 4/11/2019.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili fasaha*. Oxford University Press.

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa lugha na isimu*. Dar es Salaam University Press.

Best, J. W. & Khan, J.V. (2006). *Research in education*. (10th ed). Pearson Education inc.

Brown, G. & Yule, G. N. (1983). *Discourse analysis*. Cambridge University Press.

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English style*. Longman Group Limited.

Enon, C.J. (1998). *Education research and measurement*. Department of Distance Education, Makerere University.

Falk, J.S. (1973). *Linguistics and language. A survey of basic concept and implication*. John Wiley and sons.

Furlong, N.E, Lovelace, K.L, Lovelace, A & Lovelace, E.A. (1999). *Research methods and statistics: An intergrated approach*. Harcourt Collage Publication.

Habwe, J & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Phonixe Publishers.

Habwe, J. (1989). *Element of pragmatic discourse among mvita people*. M.A Thesis. University of Nairobi.

Habwe, J. (1999). *Discourse analysis of Swahili political Speeches*. University of Nairobi. Imepakuliwa kutoka <http://hal.cirad.fr> na imesomwa 7/10/ 2120 saa 13: 12 pm.

Kotz, S.A & Paulmann, S (2011). *Emotion, language and the brain*. Imepakuliwa kutoka <http://repository.out.ac.tz>. Imesomwa 24/07/2021 saa 08:26 am.

Paneli la Kiswahili (2019). Methali katika fasihi. Imepakuliwa kutoka <http://swa.gafkosoft.com/methali>. Imesomwa 7/11/2019 saa 22:27

Shine, M (2015). *Je, ni kweli kwamba kuvuta bangi kunaongeza akili na uwezo wa kufikiri? Makala*. Imepakuliwa kutoka <http://www.ackyshine.com>. Imesomwa 4/11/2019 saa 22:50.

ITV (2020). *Dawa za kulevya aina ya mirungi na heroini zakamatwa kwa wakati tofauti nchini*. Taarifa ya habari Septemba 28 saa 20:33.

John, E (2017). *Mbwa wakamata dawa za kulevya*. Imepakuliwa kutoka <https://www.Ippmedia.com> tarehe 26/11/2020.

Kabaleke, S. H (2020) *Mtandao wa kusambaza dawa za kulevya wanaswa*. Imepakuliwa kutoka you tube. Mwanahalisi Tv, 9/ 10, 2020.

Kothar, C.R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques (Toleo la pili)*. New Age International (P) Limited Publishers.

- Lehmann, W. P. (1962). *Historical linguistics*. Holt, Rinehart and Wiston Inc.
- Massamba, D. (2016). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B. (1987). *The impact of politics on language development in Tanzania*. Kiswahili, 54, 180 – 191.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya lugha, isimu na nadharia kwa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mdee, S.J. (1998). *Sarufi ya kiswahili sekondari na vyuo*. DUP Ltd.
- Mohammed, M.S. (2017). *Ongezeko la uingizaji na utumiaji wa madawa ya kulevya Zanzibar. Hoja binafsi ya mjumbe wa baraza la wawakilishi la Zanzibar*. Imewasilishwa Febuari, 2017.
- Nunan, D. (1972). *Research methodology in language learning*. Cambridge University Press.
- O’Grady, W., DeBrosky, M. & Katamba, R. (1997). *Contemporary linguistics. An introduction*. Longman.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya utafiti wa kitaamuli na uandishi wa tasnifu*. Cental Tanganyika Press.

- Rajab, W. T. (2017). *Tathmini ya mabadiliko ya maana ya maneno ya Kiswahili katika muktadha wa kisiasa: Mifano kutoka katika hotuba za kampeni za uchaguzi 2015*. Chuo Kikuu Huria cha Dar es Salaam.
- Sengo, (2009). *Sengo na fasihi za kinchi*, AERA Kiswahili Researched Product.
- Sign, K. (2007). *Quantitative social research methods*. India: SAGE Publication.
- Suleiman, K. A. (2015). *Kuchunguza kiwango cha mabadiliko ya matumizi ya maneno ya kipemba*. Tasnifu ya shahada ya pili. (Haijachapwa) Chuo Kikuu Huria cha Dar es Salaam.
- Tanzanian German Programme to Support Health. (2007). *Dawa za kulevya na majibu yake, kitabu cha 7*. Mkuki na Nyota Publishers Ltd.
- TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*, Oxford University Press.
- Ussi, N.H. (2014). *Matumizi ya lugha ya vijana wa kizanzibari na changamoto zake katika Kiswahili vyuo vya kati na vyuo vya vikuu*. Serengeti Educational Publishers (T).
- Verschurch P. & Doorewaard H. (2005). *Designing a research project*. Uitgeverij Lemma Publisher.
- Vestergaard I. & Shroder K. (1985). *The language of advertising*. Oxford Blackwell.
- Walliman, N. (2011). *Research methods: the basics*. Routledge Publisher
- Wamitila, K.W. (2016). *Kamusi pevu ya Kiswahili*. Vide-Muwa Publishers Limited.

Wendell, V. H. (1992). *Dictionary of concepts in library criticism and theory*. Greenwood Press.

VIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO A

MUONGOZO WA USAILI NA. 1

Maswali ya usaili kwa ajili ya wahudumu wa waathirika wa dawa za kulevya kwa ajili ya utafiti unaohusu maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Jinsi: Mwanamke () Mwanamme () Nambari ya simu.....

1. Unamfahamu muathirika wa dawa za kulevya anapozungumza?
2. Ni maneno yepi ambayo wanayatumia zaidi waathirika wa dawa za kulevya wanapozungumza?
3. Je, unaelewa maana ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya?
4. Unadhani kuna maana fiche zozote zilizomo katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya?
5. Unafikiri ni kwa nini waathirika wa dawa za kulevya hutumia maana fiche?
6. Kwa maoni yako utumiaji wa maana fiche katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya una athari gani kwa jamii ya Zanzibar?

Ahsante kwa ushirikiano

KIAMBATANISHO A

MUONGOZO WA USAILI NA. 2

Maswali ya usaili kwa askari wa kitengo cha kupambana na dawa za kulevya kwa ajili ya utafiti unaohusu maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Jinsi: Mwanamke () Mwanamme () Nambari ya simu.....

1. Unamfahamu muathirika wa dawa za kulevya anapozungumza?
2. Ni maneno yepi ambayo wanayatumia zaidi waathirika wa dawa za kulevya wanapozungumza?
3. Je, unaelewa maana ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya?
4. Unadhani kuna maana fiche zozote zilizomo katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya?
5. Unafikiri ni kwa nini waathirika wa dawa za kulevya hutumia maana fiche?
6. Kivipi maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya unaathiri harakati za mapambano dhidi ya dawa za kulevya?

Ahsante kwa ushirikiano

KIAMBATANISHO A

MUONGOZO WA USAILI NA. 3

Maswali ya usaili kwa walimu wa skuli teule kwa ajili ya utafiti unaohusu maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Jinsi: Mwanamke () Mwanamme () Nambari ya simu.....

1. Unamfahamu muathirika wa dawa za kulevya anapozungumza?
2. Je, unawafahamu wanafunzi wanaojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya?
3. Ni maneno yepi ambayo wanayatumia zaidi wanafunzi ambao ni waathirika wa dawa za kulevya?
4. Unadhani kuna maana fiche zozote zilizomo katika maneno yanayotumiwa na wanafunzi hao?
5. Je, unaelewa maana fiche za maneno yanayotumiwa na wanafunzi waathirika wa dawa za kulevya?
6. Unafikiri ni kwa nini hutumia maneno yenye maana fiche?
7. Nini athari ya matumizi ya maana fiche katika maneno yanayotumiwa na wanafunzi wanaotumia dawa za kulevya?

Ahsante kwa ushirikiano

KIAMBATANISHO A

MUONGOZO WA USAILI NA. 4

Maswali ya usaili kwa wazazi/walezi wa wanafunzi kwa ajili ya utafiti unaohusu maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

Jinsi: Mwanamke () Mwanamme () Nambari ya simu.....

1. Unamfahamu muathirika wa dawa za kulevya anapozungumza?
2. Ni maneno yepi ambayo wanayatumia zaidi waathirika wa dawa za kulevya wanapozungumza?
3. Je, unaelewa maana ya maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya?
4. Unadhani kuna maana fiche zozote zilizomo katika maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya?
5. Unafikiri ni kwa nini waathirika wa dawa za kulevya hutumia maana fiche?
6. Ukiwa mzazi/mlezi unadhani jamii inaathirika vipi na maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya?

Ahsante kwa ushirikiano.

KIAMBATISHO B**MUONGOZO WA MJADALA WA KUNDI LENGWA**

Muongozo wa mjadala kwa ajili wa waathirika wa dawa za kulevya waliopo katika nyumba za kurekebisha tabia za waathirika wa dawa za kulevya na kliniki za waathirika wa dawa za kulevya. Muongozo huu ni kwa ajili ya utafiti unaohusu maana fiche za maneno yanayotumiwa na waathirika wa dawa za kulevya Zanzibar.

1. Inasemekana mnatumia zaidi maneno yenye maana fiche katika mazungumzo yenu. Ni kweli?
2. Mnaweza kunitajia maneno kadhaa ambayo mnayatumia yenye maana fiche?
3. Mmeficha maana zipi katika maneno hayo?
4. Kwa nini mnafanya hivyo?
5. Kufanya hivyo kunakusaidieni nini?
6. Msipotumia maneno kama hayo mtapata changamoto gani?

Ahsante kwa ushirikiano

KIAMBATISHO C

ORODHA YA MANENO YENYE MAANA FICHE YALIYOTAFITIWA

Na.	MANENO	MAANA FICHE
1	<i>Nambwinya</i>	Kusumbua
2	<i>Ngada</i>	Unga (dawa ya kulevya)
3	<i>Sembe</i>	Unga wa awa ya kulevya
4	<i>Mihemo</i>	Pesa
5	<i>Mabovu</i>	Kukosa pesa
6	<i>Mazuri</i>	Kuwa na pesa.
7	<i>Bomu</i>	Bangi
8	<i>Sumu</i>	Unga (dawa ya kulevya)
9	<i>Dawa</i>	Unga (dawa ya kulevya)
10	<i>Roho inapenda</i>	Unga (dawa ya kulevya)
11	<i>Kudaka sumu</i>	Kuvuta unga.
12	<i>Maji</i>	Gongo

13	<i>Wazee</i>	Askari
14	<i>Njaa kali</i>	Askari
15	<i>Wachawi</i>	Askari
16	<i>Wadudu</i>	Askari
17	<i>Geto</i>	Kituo cha polisi
18	<i>Kitunduni</i>	Rumande
19	<i>Gontenamu</i>	Chumba katika kituo cha polisi kinachotumika Kuwahoji watuhumiwa
20	<i>Arifu</i>	Rafiki ambaye ni mtumiaji wa dawa za kulevya
21	<i>Adimu</i>	Rafiki ambaye ni mtumiaji wa dawa za kulevya
22	<i>Chafu</i>	Rafiki ambaye ni mtumiaji wa dawa za kulevya
23	<i>Brauni</i>	Unga wenye rangi ya udongo (katika hali ya jiwe)
24	<i>Pele</i>	Unga wenye rangi nyeupe (katika hali ya jiwe)
25	<i>Kraki,</i>	Unga wenye rangi ya nyeupe (katika hali ya jiwe)
26	<i>Kichupa,</i>	Unga wenye rangi ya nyeupe (katika hali ya jiwe)
27	<i>Musharafu</i>	Unga wenye rangi ya samli

28	<i>Skanka</i>	Bangi nzuri.
29	<i>Kizidrai</i>	Bangi ambayo haijachanganywa na kitu chengine.
30	<i>Msokoto</i>	Mchanganyiko wa bangi na unga.
31	<i>Pafu</i>	Kuvuta bangi.
32	<i>Kipusa</i>	Muuza unga.
33	<i>Chaukucha</i>	Bangi iliyobaki kipande kidogo kisichoweza kushikika vizuri.
34	<i>Farasi</i>	Gari la polisi
35	<i>Arosto</i>	Maumivu anayoyapata mtumiaji wa dawa za kulevya anapokosa dawa hizo.
36	<i>Mtambo</i>	Gongo
37	<i>Pusha</i>	Muuza unga
38	<i>Dokta</i>	Muuza unga
39	<i>Mkali wao</i>	Muuza unga
40	<i>Faza</i>	Muuza unga
41	<i>Mzungu</i>	Muuza unga

42	<i>Sadari</i>	Muuza unga
43	<i>Mzee wa utamu</i>	Muuza unga
44	<i>Mwana</i>	Mtumiaji wa dawa za kulevya.
45	<i>Mshindo</i>	Pesa nyingi za wizi
46	<i>Rizla</i>	Bangi
47	<i>Pepa</i>	Karatasi ya kusokotea banngi
48	<i>Waiti</i>	Karatasi ya kusokotea banngi
49	<i>Sanda</i>	Karatasi ya kusokotea banngi
50	<i>Nguo</i>	Karatasi ya kusokotea bangi.
51	<i>Mchokocho</i>	Mbegu za bangi
52	<i>Majani</i>	Bangi
53	<i>Haba</i>	Bangi
54	<i>Kwida</i>	Bangi
55	<i>Blandi</i>	Bangi
56	<i>Kaya</i>	Bangi

57	<i>Chicha</i>	Bangi
58	<i>Mtorijo</i>	Bangi
59	<i>Widi</i>	Bangi
60	<i>Stiki</i>	Bangi
61	<i>Aguli</i>	Bangi
62	<i>Msuba</i>	Bangi
63	<i>Dongo</i>	Bangi
64	<i>Tembele</i>	Mirungi
65	<i>Chakusaga</i>	Mirungi
66	<i>Njugu</i>	Vidonge vya kulevya
67	<i>Karanga</i>	Vidonge vya kulevya
68	<i>Vyakudanki</i>	Vidonge vya kulevya
69	<i>Nomemori</i>	Vidonge vya kulevya
70	<i>Shwaini</i>	Vidonge vya kulevya
71	<i>Kwarukwaru</i>	Vidonge vya kulevya

72	<i>Njunja</i>	Vidonge vya kulevya
73	<i>Chuma</i>	Gongo
74	<i>Ngumu Kumeza</i>	Gongo
75	<i>Kosovo</i>	Eneo linalouzwa pole.
76	<i>Kachaso</i>	Pombe
77	<i>Jojiwea</i>	kipimo cha pombe lita moja na nusu
78	<i>Jibuti</i>	Kipimo cha pombe glasi moja iliyojaa,
79	<i>Nusu</i>	Nusu glasi ya pombe
80	<i>Nibu</i>	Robo glasi ya pombe
81	<i>Supu ya mawe</i>	Gongo
82	<i>Hashi</i>	Charas
83	<i>Gundi</i>	Charas
84	<i>Chapori</i>	Pombe
85	<i>Doriani</i>	Mpelelezi
86	<i>Yakumwaga</i>	Yenye kutosheleza

87	<i>Mwari</i>	Mtu asiyevuta bangi
88	<i>Mdananda</i>	Mtu asiyetumia unga
89	<i>Kumbi</i>	Mtu asiyetumia dawa yoyote ya kulevya likimfananisha na mwanaume shoga
90	<i>Kupendeza</i>	Hali inayomtokea mtu baada ya kutumia dawa za kulevya.
91	<i>Maziwa</i>	Manii
92	<i>Mukide</i>	Poa
93	<i>Cheua</i>	Toa pesa au mali uliyonayo.
94	<i>Tapika</i>	Toa pesa au mali uliyonayo.
95	<i>Boga</i>	Mtu asiyetumia unga
96	<i>Nyuki</i>	Kipande kidogo cha msokoto wa bangi kilichobaki
97	<i>Kicha</i>	Fungu la mirungi
98	<i>Nyongo</i>	Bangi iliyotengenezwa kwa mfumo wa sigara
99	<i>Busta</i>	Kidonge kimoja cha dawa za kulevya.
100	<i>Njumu</i>	Bangi

101	<i>Mdude</i>	Bangi mbichi
102	<i>Ndonga</i>	Mchanganyiko wa bangi na unga
103	<i>Mwanamke wa kihindi</i>	Unga
104	<i>Kujishuti</i>	Kujidunga sindano ya dawa za kulevya.
105	<i>Kuyoyoma</i>	Usingizi unaotokanana dawa za kulevya.
106	<i>Taita</i>	Muuza bangi au mirungi

Chanzo: Data kutoka uwandani.

KIAMBATISHO D**BAJETI YA UTAFITI**

Na	Tukio/Vifaa	Idadi	Gharama @	Jumla
01	Kompyuta	1	950,000/=	950,000/=
02	Vidaftari vya kuhifadha data	05	1000/=	5,000/=
03	Kalamu	10	1000/=	10,000/=
	Mstari	01	500/=	500/=
04	Kinasa sauti	1	200,000/=	200,000/=
05	Flashi	1	20,000/=	20,000/=
06	Kuprinti na kutolesha nakala	Nakala 10	Ukurasa Tsh. 500/=	Tsh. 200,000/=
Chakula				
07	Chakula cha asubuhi	Siku 60	Tsh.5000/=	Tsh. 300,000/=
08	Chakula cha mchana	Siku 60	Tsh. 7000/=	Tsh. 420,000/=
Usafiri na Mawasiliano				
09	Usafiri kwenda na kurudi uwandani	Siku 60	Tsh. 3000/=	Tsh 180,000/=
10	Mawasiliano kwa msimamizi	wiki 28	Tsh. 2,000/=	Tsh.56,000/=

11	Mawasiliano kwa watafiti wasaidizi na watoa taarifa	Wiki 8	Tsh. 5,000/=	Tsh.40,000/=
Posho ya Mtafiti Msaidizi				
12	Watafiti wasaidizi	3	Tsh. 10,000/=	Tsh. 30,000/=
13	Wahudumu	10	Tsh. 10,000/=	Tsh. 100,000/=
14	Wazazi/walezi	18	Tsh. 10,000/=	Tsh. 180,000/=
15	Waathirika wa dawa za kulevya	40	Tsh. 5000/=	Tsh. 200,000/=
Dharura				150,000/=
Jumla Kuu				TSH. 3,041,500 /=

KIAMBATISHO E**RATIBA YA UTAFITI**

Na	Tukio	Kuanzia	Mpaka
1	Ukusanyaji wa data.	Juni, 2020	Ogasti, 2020
2	Uchambuzi wa data.	Agosti, 2020	Novemba, 2020
3	Uandishi wa tasnifu.	Disemba, 2020	Januari, 2021
4	Uwasilishaji tasnifu kwa mara ya kwanza na marekebisho	Januari, 2021	May, 2021
5	Uwasilishaji wa tasnifu kwa Kurugenzi ya Masomo ya Juu na Utafiti	Julai, 2021	
6	Utetezi wa tasnifu	Novemba, 2021	
7	Marekebisho baada ya utetezi		Novemba, 2021
8	Uwasilishaji wa tasnifu ya mwisho		Disemba, 2021